ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu

49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu – Tarehe 5 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ahsante sana kwa heshima na ruhusa yako, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Kuweka Utekelezaji wa Majukumu na Uwezo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Kuweka Utekelezaji wa Majukumu na Uwezo na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 16

Vikao vya Kutatua Kero za Muungano

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali inayo dhamira njema ya kuondoa kero za muungano kwa kuunda Kamati Maalum inayoongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Kiongozi wa pili katika Serikali ya Muungano.

(a) Je, hadi sasa ni kero ngapi za muungano tayari zimepata ufumbuzi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

(b) Je, vikao vya kuondoa kero za muungano mwaka 2012 vimeshafanyika vingapi Tanzania Bara na Zanzibar.

(c) Tokea vikao hivi viasisiwe ni kiasi gani cha fedha za wananchi zimetumika kuviratibu na kuvigharamia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zina nia thabiti ya kuondosha kero zote za Muungano, ili kuimarisha Muungano wetu na kuhakikisha kuwa haki ya kila upande wa Muungano inapatikana bila ya upendeleo, na wananchi wanafanya shughuli zao bila ya matatizo.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameunda Kamati ya Pamoja inayoongozwa na Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano inayowajumuisha Wajumbe kutoka SMT na

SMZ inayoshughulikia changamoto mbali mbali za Muungano kwa kuzipatia ufumbuzi unaofaa kwa kujadiliwa katika ngazi mbali mbali.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, tokea kuanzishwa utaratibu wa kuzitafutia ufumbuzi changamoto za Muungano, jumla ya hoja za Muungano (13) zimewasilishwa katika vikao vya pamoja vya SMZ na SMT. Kati ya hizo hoja 6 tayari zimeshapatiwa ufumbuzi, hoja 3 zimo katika hatua za kupatiwa ufumbuzi na hoja 4 zinaendelea kupatiwa ufumbuzi.

(b) Mhe. Spika, katika mwaka 2012 jumla ya vikao 19 vya kutatua changamoto za Muungano vimefanyika. Kati ya hivyo, vikao tisa (9) vya Sekretarieti, vinne (4) vya Makatibu Wakuu, vikao viwili (2) kwa ngazi ya Mawaziri na vikao viwili (2) ni vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ na vikao hivyo vilifanyika Zanzibar na Dar-es-Salaam kwa ridhaa ya pamoja.

(c) Mhe. Spika, vikao vya kujadili changamoto za Muungano, kuanzia ngazi ya Makatibu Wakuu, Mawaziri hadi Kamati ya Pamoja huwa vinagharamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha vikao vya kisekta vinavyofanyika, sekta husika inagharamia wataalamu wake kwa vikao hivyo. Hivyo sio rahisi kwa Ofisi yangu kupata matumizi ya kila sekta kwenye kila kikao tokea kuasisiwa vikao hivi mwaka 2006.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana kabisa ya Mhe. Waziri.

Kwa kweli changamoto kubwa ya wananchi wa Zanzibar kuhusu suala la mafuta na utafiti.

(a) Je, ni lini suala hili litamalizika, ili kutoa fursa kwa wawekezaji kuja kuwekeza kwa haraka.

(b) Kumekuwa na kilio kikubwa sana cha wazanzibari kutozwa kodi mara mbili Tanzania Bara na hichi kilio sijui kitamalizika lini, ili wazanzibari wapate kupumua nao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kabla ya kumjibu naomba lile swali la mwanzo alirudie kuhusu mafuta na utafiti au mafuta na gesi asilia sikusikia vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, swali la mwanzo ni kuhusu suala la utafiti wa mafuta, jambo hili litamalizika lini na jengine ni kuhusu ulipaji wa kodi mara mbili kwa wafanyabiashara wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu suala la mafuta na gesi asilia, kwa kweli jambo hili kama anavyojua ni moja miongoni mwa mambo ya Muungano na kutokana na uamuzi wa Baraza hili tukufu liliamuliwa kwamba jambo hili litolewe kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Vikao mbali mbali Mhe. Spika vimekaa katika kutoa jambo hili katika orodha ya mambo ya Muungano na hivi sasa tuko katika hatua ya mwisho.

Kwa hivyo, hivi sasa imeundwa Kamati Maalum ya Wanasheria Wakuu kutoka pande zetu mbili kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi tatizo hili, kwa sababu ni tatizo ambalo linaguswa na utata wa kisheria, utata wa kitaalamu, mipaka na kadhalika. Kwa maana hiyo, Kamati yetu hii ya Wanasheria Wakuu wanakaa kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi, ili utekelezaji utakapokuwa tayari usiwe na tatizo.

Hivyo, tuko kwenye hatua ya mwisho na ninamuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi waendelee kuvuta subira kwa kuwa jambo hili liko katika hatua za mwisho za kukamilika.

Kuhusu suala la kodi ya mara mbili Mhe. Spika, jambo hili limezungumzwa na kwa ufupi kama limepatiwa ufumbuzi, isipokuwa tatizo limebakia kidogo katika utekelezaji kwa upande wetu wa Zanzibar, ambapo tunatakiwa sote wakati bidhaa inapoingia tuwe na utaratibu wa kuwa na *pre inspection*, ili hizo hatua za ulipaji wa kodi uwe sawia kwa kila upande.

Kwa hivyo, tumo kwenye hatua za mwisho za kulimaliza tatizo hili, ili wananchi wetu nao wasipate bughudha ya aina yoyote wakati wanapopeleka bidhaa zao huko Tanzania Bara. Kwa ufupi limo kwenye hatua za mwisho na wakati wowote litapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na Mhe. Waziri amesema kwamba kuna kero ambazo zimetatuliwa, isipokuwa bado kuna kero nne zenye *concept* ya uchumi ndani yake ikiwemo Mfumo wa Hazina wa Pamoja bado halijatatuliwa. Je, kero hii itapatiwa ufumbuzi lini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli suala la Tume ya Pamoja ni la muhimu sana katika kutatua masuala matatu ya kiuchumi katika Jamhuri yetu ya Muungano. Kwa hiyo, naamini mara itakapopatikana ufumbuzi wa tatizo hili, basi mambo mbali mbali ambayo ni ya kiuchumi na kimapato katika Jamhuri ya Muungano matatizo hayo yatakuwa yameondoka.

Kwa maana hiyo, nataka nimhakikishie kwamba tume hii imo katika hatua za mwisho kumaliza kila kikwazo, ili upatikane ufumbuzi na Zanzibar tayari imeshatoa maoni yao katika suala hili la Tume ya Pamoja na tulikuwa tunasubiri wenzetu kwa upande wa Tanzania Bara. Sasa na wao tayari Kikao cha Baraza la Mawaziri kimekaa na hivyo hili limo kwenye hatua za mwisho kwa ajili ya kulimaliza tatizo hili na sasa lisiwe tena ni tatizo kwenye kero za Muungano.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Waziri alisema kwamba kuna hoja 6 tayari zimetatuliwa, 3 zinaendelea na 4 bado.

(a) Kwa hivyo, mimi nataka atufafanulie atutajie hizo hoja ambazo tayari zimeshatatuliwa 6, 3 ambazo zinaendelea na zile 4 ambazo zinasubiri.

(b) Nataka kujua hizi hoja mpaka lini zitakuwa zimekwisha kutatuliwa, maana yake kila siku zinaonekana zinaendelea na kila tukenda siku zinaendelea. Sasa hebu tujue hasa lini kero hizi zitakuwa zimeshatatuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu hoja ambazo zimepata utatuzi ni hizi zifuatazo:-

1. Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binadamu Zanzibar na uwezo wa Zanzibar kujiunga na *IMO*.
2. Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje.
3. Misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IMF* kuhusu matumizi ya *MDRI*.
4. Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.
5. Mgawanyo wa Kodi *Payee* zinazotokana na wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar.
6. Uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, kwa yale ambayo yamo kwenye hatua ya mwisho ni pamoja na:

(i) Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili.
(ii) Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu.
(iii) Ajira ya Wawakilishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano.

Vile vile kwa yale ambayo yanayoendelea kupatiwa ufumbuzi ni haya yafuatayo:-

(a) Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki.
(b) Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.
(c) Hisa za SMZ zilizokuwa kwenye Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki na
(d) Mgawanyo wa mapato yanayotokana na faida ya *BoT*.

Mhe. Spika, kuhusu lini yatamalizika matatizo haya. Kwa kweli matatizo ndio mchakato wa maisha, kwa sababu yatamalizika hapa na mengine yatajitokeza. Kwa hivyo, kusema lini tutamaliza si rahisi Mhe. Spika, isipokuwa jitihada zinafanywa na serikali kuhakikisha kwamba kila tatizo tunalitatua kwa maslahi ya kuyapatia ufumbuzi matatizo ya wananchi, ili wananchi waweze kuishi vizuri zaidi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na hatua zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha kwamba nia na dhamira ni kuondosha kero na matatizo yanayojitokeza.

Nam. 89

Utaratibu Unaotumika Kuendesha Mwenge wa Uhuru

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Suala la Mwenge wa Uhuru, tangu zamani na hadi sasa linachukuliwa kuwa ni jambo la kitaifa, kwa msingi huo mbio pamoja na shughuli zake zote huendeshwa kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii bila kujali itikadi za kisiasa au jiografia mtu anayotoka.

(a) Ni utaratibu gani unaotumika katika uteuzi wa Mkuu wa mbio za mwenge.

(b) Kuna utaratibu gani unaotumika katika kuzindua na kusaidia miradi mbali mbali baina ya pande mbili hizi za Muungano.

(c) Gharama zinazotumika katika mbio za mwenge hutoka SMT au na SMZ nayo huchangia.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Mwenge wa Uhuru ni jambo la kitaifa na shughuli zake zote zinaendeshwa kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii na baadhi ya wafadhili.

(a) Mhe. Spika, utaratibu unaotumika kuwapata wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa akiwemo Kiongozi wa Mbio hizo, Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto huwa inawatangazia vijana wote, ambao ni raia wa Tanzania wenye sifa zinazohitajika kama vile afya njema, waliomaliza darasa la kumi na mbili na kuendelea na walio na umri kuanzia miaka 18 hadi 35 kuomba nafasi hizo.

    Baada ya kupokea maombi vijana hao hufanyiwa usaili na Kamati Maalum iliyoteuliwa na Wizara yenye uzoefu wa kukimbiza mwenge kitaifa. Utaratibu wa kumpata kiongozi wa wawakimbiza mwenge ni kwamba kila mwaka tunapokezana baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, utaratibu unaotumika wa kuzindua mbio za mwenge na kilele chake ni mikoa yenyewe ndio inayoomba kwa uongozi wa wizara baada ya wizara kuridhika na sababu za maombi yao, basi mkoa ndio unapewa fursa ya kuandaa uzinduzi au sherehe za kilele.

    Kwa upande wa uzinduzi na kusaidia miradi mbali mbali ni uongozi wa mkoa ndio unaohamasisha wananchi kuchangia miradi yao tofauti, ambapo mbio za mwenge hupita kuzindua au kuweka mawe ya msingi. Kwa hivyo, wingi na uchache wa miradi hutegemea sana jinsi ya uhamasishaji unaofanywa na viongozi wa mkoa. Aidha wilaya inayoshinda kitaifa huwa inazawadiwa.

(c) Gharama kubwa zinazotumika katika mbio za mwenge hutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huchangia gharama za uendeshaji wa mbio za mwenge katika mikoa ya Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kwa idhini yako kabla ya kuuliza swali la nyongeza nimpongeze Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej pamoja na Mama Ndimimi yule Mama wa Kimasai kwa kuweza kupata nishani ya Mwanamke Jasiri, kwa kweli nishani hii Wamarekani wamesibu kwa sababu huyu mama mbali na ujasiri wake katika kutetea Zanzibar ni jasiri sana katika kuwatetea wananchi kwa jumla ahsante sana Mama Fatma Abdulhabib Ferej. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye swali la nyongeza kama ifuatavyo. Uzoefu unaonesha kwamba viongozi wa mbio za mwenge mara nyingi huwa wanatoka Tanzania Bara, na kwa kuwa wazanzibari na wao hulipia gharama hizi kama wanavyolipia wenzao.

(a) Je, hakuna utaratibu maalum unatumika kui-*alternate* nafasi ya kiongozi wa mbio za mwenge kwamba mwaka atoke Bara na mwaka mwengine atoke Zanzibar.

(b) Kwa kuwa vyama vya siasa vipo hapa kwa mujibu wa Sheria Nam. 5 ya mwaka 1992. Je, ni mwaka gani kiongozi wa mbio za mwenge alitoka vyama vya upinzani ukiachia CCM.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa kweli swali la (b) sikulisikia vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali la (b).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana naomba nirejee swali la (b), ili mama yangu pale aweze kunisikia vizuri sana. Kwa kuwa vyama vya siasa vipo kwa mujibu wa Sheria Nam. 5 ya mwaka 1992.

Je, ni mwaka gani kiongozi wa mbio za mwenge aliyetoka katika vyama vya upinzani kwa maana ya CHADEMA, *CUF* na vyenginevyo ukiachia mbali hichi chama chetu cha CCM.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba nimjibu swali la (a) ambalo nimelipata vizuri sana. Kwa hivyo, naomba nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba kuna utaratibu maalum wa kuchagia viongozi wa kukimbiza mbio za mwenge na kwa kweli kila mwaka tunabadilishana. Kwa mfano, mwaka jana kiongozi alitoka Tanzania Bara, lakini mwaka huu kiongozi atatoka hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niongezee nyongeza ndogo.

Mhe. Spika, kwa utaratibu hivi sasa mbio za mwenge hazisimamiwi tena na vyama vya siasa, bali mbio za mwenge zinasimamiwa na serikali, yaani ni suala la kitaifa. Kwa hivyo, utaratibu wake wa kuchagua kiongozi wa mbio za mwenge unatokana kama ambavyo Mhe. Waziri ameeleza.

Hivyo, napenda kumueleza Mhe. Mwakilishi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwamba anayechaguliwa hatokani kwa maana ya uasili wa vyama vya siasa, isipokuwa huchaguliwa kama ni Mzanzibari ama ni mwenzetu kutoka upande wa Tanzania Bara aongoze mbio hizi za mwenge kama ni jambo la kitaifa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, ahsante nashukuru kupata nafasi hii na mimi nikaweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la mbio za mwenge ni jambo la Muungano wizara na taasisi za serikali pamoja na za watu binafsi huchangia mbio hizo.

Je, ni utaratibu gani unaotumika kwa kupatikana michango hiyo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, inavyotakiwa taasisi pamoja na wananchi wote wauchangie mwenge na wala hauna itikadi kama alivyokwisha kusema pale Mhe. Waziri.

Lakini fedha zikeshapatikana katika mikoa au wilaya zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo. Kwa hivyo, kadri Mhe. Mwakilishi utakavyojitahidi kuleta maendeleo katika jimbo lako ndivyo kadri utakavyopata mchango mkubwa wa mwenge.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri huu mwenge kitaifa mwaka huu unategemewa kuwashwa mkoa gani.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, mwaka huu mwenge utawashwa katika Mkoa wa Kusini Pemba katika kijiji cha Chokocho. *(Makofi)*

Nam. 25

Uzio wa Kiwanja cha Ndege Zanzibar

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Uzio unaouzunguka Kiwanja cha Ndege Zanzibar hivi sasa umefikia karibu na eneo la Kisauni na ujenzi unaoendelea, unaonekana kama kwamba uzio ulioanza kujengwa mwanzo haukupita inavyotakiwa.

(a) Wananchi ambao wameathirika na ujenzi huo watalipwa fidia.

(b) Utaratibu gani utatumika katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata fidia zao kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika ujenzi wa uzio kwa awamu ya kwanza malipo ya fidia kwa wananchi tayari yamelipwa yote. Kwa awamu ya pili, ambapo mpaka sasa ujenzi wa uzio umeshafanyika kwa urefu wa kilomita 1.2km kati ya kilomita 6km na tupo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha malipo hayo. Jumla ya shilingi milioni 120 zimetengwa kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo.

(b) Utaratibu unaotumika ni wa kawaida wa serikali wa kuhakiki na kutathmini kisha baadae kulipwa fidia kwa wale wanaostahiki. Njia za malipo zinazotumika ni kwamba kwenye mkataba wa ujenzi wa ukuta, kuna fedha maalum tayari zimetengwa kwa ajili ya kulipia fidia za mazao sehemu inayopita ukuta huo.

Baada ya tathmini kufanyika mkandarasi analipa moja kwa moja kwa muhusika, kwa malipo makubwa kama vile nyumba na vyenginevyo serikali ndio inayobeba dhamana. Aidha hakuna nyumba ya mwananchi yeyote itakayovunjwa kabla muhusika kulipwa fidia stahiki.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata majibu ambayo ni mazuri kuhusiana na swali hili, lakini ninalo swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, tukiangalia uzio huu niliouzungumza kwa upande huu wa Kisauni au barabara inayoelekea Kisauni umejengwa kiasi ambacho na huku kulikoanza mwanzo haukufungana, yaani sehemu moja iko nje na nyengine iko ndani na katikati kuna nyumba na uwazi wa kutosha wa mtu kupita na kila kitu. Madhumuni ya uwanja huu ilikuwa ujengwe kwa kuzuia mambo yote yasiingie kwa usalama wa kiwanja pamoja na ndege zinazotua na kuruka.

(a) Kwa nini uzio huu ukaacha nafasi mbili kubwa namna ile na wala haukufungana na ukawa kitu kimoja.

(b) Zile nyumba zilizopo baina ya ukuta huu ulikofika kwenye barabara inayoelekea Kisauni na huku ulikojengwa mwanzo nyumba zile ina mpango gani wa kutolewa fidia na kulipwa halafu ule ukuta ufunganishwe au hali ile ndio imeshamaliza.

(c) Kwa sababu sivyo nina hakika ramani ilivyokusudiwa kujengwa vile. Je, ni hasara gani imepatikana katika kujenga ukuta katika hali ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la ujenzi wa ukuta wa uwanja wa ndege ni jambo ambalo limejengewa hatua baada ya hatua. Hatua ya awali ilitokana na mradi wa *run way*, wakati unaanza kujengwa ukuta upande wa mashariki, yaani huo upande wa Kisauni, basi ukuta ule ulijengwa bila ya kuzingatia eneo la uwanja wa ndege.

Sasa katika mradi wa hatua ya pili ukuta unaojengwa umezingatia katika mipaka ya eneo la uwanja wa ndege. Hivyo, basi maeneo ambayo anahisi au ameyaona Mhe. Mwakilishi kwamba yameachana, sababu ya msingi ni kwamba ukuta wa kwanza ulilenga kuzuia watu, wanyama na vitu vyenginevyo visiingie kwenye eneo la uwanja wa ndege. Ukuta wa pili una madhumuni ya kuzuia eneo husika la uwanja wa ndege.

Matarajio yetu ni kwamba baada ya kukamilisha ukuta wetu huu wa hatua ya pili unaohifadhi eneo la uwanja wa ndege, basi tutaupachua ukuta ule ulioko upande wa mashariki, ili kuendana na ukuta huu ambao tunajenga hatua ya pili.

Aidha katika kipindi hiki eneo lile ambalo ukuta ule haujafika tumeshajiandaa na kuweka senyenge ili kuzuia wanyama, watu na vitu vyenginevyo visiingie katika uwanja wa ndege ili kunusuru na kukinga hatua za usalama.

Swali la pili Mhe. Spika, nyumba anazosema Mhe. Mwakilishi kuna nyumba ambazo ni za serikali zilizokuwa zikitumika na Kampuni ya Kiboko ambazo ziko chini ya Wizara ya Miundombinu hivi sasa hizo haziko katika utaratibu wa fidia. Kama kuna nyumba ya mwananchi yeyote iliyo katika eneo la Uwanja wa Ndege azma ya serikali kwamba hatutovunja nyumba hiyo kabla ya kumlipa fidia, tumevunja nyumba mbili ambazo tayari tumeshazilipa fidia. Nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hakuna mtu ambaye atapoteza haki yake kwa kuvunjwa nyumba yake bila ya kulipwa fidia.

Mhe. Spika, swali la tatu, katika ujenzi huu mpaka muda huu hatujaona kama kuna hasara zaidi ya faida ambazo zitapatikana kwa kuimarisha usalama na ulinzi kwa eneo lote la Uwanja wa Ndege. Hivi sasa tumejenga takriban kilomita 7.3 tumebakisha karibu kilomita 4.8 matarajio yetu kwamba tukikamilisha kilomita hizo nne tutakuwa tayari tume-*cover* eneo lote la Uwanja wa Ndege na itakuwa tayari tuko katika hatua ya mwisho kukidhi matakwa na masharti ya usalama kwa viwanja vya ndege.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, karibuni tulikuwa na ripoti ya Kamati Teule kuhusu Uwanja wa Ndege juu ya ulipaji wa fidia kwa watu waliolalamika kuhusu kulipwa fidia. Lakini wakati huo huo Uwanja wa Ndege upande wa Kusini/Magharibi bado kuko wazi hakujajengwa uzio wa kufidia ule uwanja na wakati serikali ililipa fidia wananchi eneo hilo na sasa hivi serikali bado haijakujenga kuko wazi na wananchi wanavamia na kuingia.

Je, hatuoni kama kukuacha wazi ikawa hakujajengwa serikali italipa fidia mara zote ikenda ikirudi na kulipa tena. Na kama hivyo ndivyo, ni lini upande wa Kusini/Magharibi kwa uwanja kutajengwa uzio ili serikali isipate gharama mara tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, upande wa Kusini/Magharibi ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar takriban kuna miradi mitatu ambayo inaendelea, kuna mradi wa *terminal, Apron* na *Tax way* na kuna mradi wa ukuta. Fidia ambayo ilikuwa imelipwa ilikuwa inahusiana na suala la *terminal, Apron na Tax way*. Suala la mradi wa ukuta eneo la upande wa Kusini/Magharibi ya uwanja hatujalipa fidia, tumetenga jumla ya shilingi 120 milioni tutawalipa wenyewe na ukuta wetu utapita ili kukidhi mahitaji ya ujenzi kwa kuhifadhi uwanja wetu wa ndege.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, lakini kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 34 naomba niseme machache. Kwa masikitiko makubwa pamoja na juhudi anazozichukua Mhe. Rais kuhusu wananchi wake wa Visiwa vya Unguja na Pemba bado kumekuwa na kitendawili cha uzazi kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja, mpaka hivi sasa ninavyozungumza wazazi bado wanachangishwa huduma hiyo na hii ni hatari na Kamati iliagiza suala hili. Baada ya hayo sasa naomba Mhe. Spika, swali langu Nam. 34 lipate jawabu.

Nam. 34

Tunzo ya Kutokomeza Malaria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mwanzoni mwa mwezi wa Februari 2012, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alipewa tunzo nchini Ethiopia kwa Tanzania kufanikiwa kutokomeza malaria.

(a) Je, ni taasisi ipi na ya nchi gani iliyofanya tathmini na kuonesha kuwa ugonjwa wa malaria umepungua kwa kiasi cha nchi kupewa tunzo.

(b) Je, hivi sasa ugonjwa huo upo kwa kiwango gani nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukizungumza nchi tunazungumza Tanzania yaani Tanzania Bara na Zanzibar. Mhe. Spika, suala la afya sio suala la Muungano, Tanzania na Zanzibar tuna wizara mbili tofauti kwa hivyo kuna taarifa tofauti za Tanzania na taarifa za Zanzibar. Kwa vile Mhe. Mwakilishi pia ni Mbunge na anataka taarifa za takwimu za Tanzania ningemshauri akaulizie Bungeni kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wa Tanzania kama anao ubavu. Lakini kama anataka taarifa za takwimu za Zanzibar ambazo nina mamlaka nazo hilo naweza kulisemea. Sasa anataka za Zanzibar au anataka za Tanzania.

Mhe. Spika: Hebu jibu kwa namna ulivyojitayarisha majibu yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kujibu taarifa za Zanzibar. Ningependa kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

Kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alipewa tunzo nchini Ethiopia kwa ajili ya sehemu moja ya Tanzania kufanikiwa kupunguza kiwango kikubwa cha malaria lakini bado hayajatokomezwa, sehemu hiyo itakuwa ni Zanzibar. Kitengo cha Malaria, *Zanzibar Malaria Control Program*, ndio taasisi inayohusika na kufanya tathmini ya kiwango cha malaria Zanzibar kwa kufanya tafiti, *Malaria Indicator Survey*.

Global Fund kwa mashirikiano na *Present Malaria Initiative* wamekuwa wakifadhili utekelezaji wa kazi hizi hapa Zanzibar, tathmini ilifanyika mara mbili mwaka 2007 na 2010 kupitia kwenye jamii na baadhi ya Vituo vya Afya vilivyochaguliwa kutoka katika Wilaya kumi za Unguja na Pemba, ili kuangalia kiwango cha malaria Zanzibar. Matokeo ya kiwango cha malaria kwa mwaka 2007 yalikuwa 0.8 wakati mwaka 2010 – 2012 taarifa za kitengo zinaonesha kwamba malaria ilishuka kufikia 0.07.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri ya kusikitisha na ambayo hayana mshiko na nafikiri haujui wajibu wake kama yeye ni Naibu Waziri. Mimi ni Mbunge nawashukuru Wajumbe walionichagua kwenda Bara na hili suala nimekuja hapa kuwakilisha wananchi sio suala la Bunge ajuwe wajibu wake.

Mhe. Spika, suala la takwimu kimataifa ni orodha ya mambo ya Muungano na kama ni ya Muungano katika kipindi kilichopita niliuliza swali hapa mimi la Babu wa Loliondo na alinijibu yeye huyo Mhe. Naibu Waziri, sasa sioni sababu ya kunijibu swali hili kiufasaha kabisa.

Mhe. Spika: Uliza swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kumekuwa na vipimo katika hospitali ya Mnazi Mmoja ukenda kuchunguza Malaria yanakuwa hayaonekani, ukenda hospitali binafsi yanaonekana ukiangalia vipimo vile vyote vya aina moja moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Wizara ya Afya inataratibu zake za kuchunguza malaria. Tuna njia mbili, tunachukunguza kwa darubini na tunachunguza na kipimo kinaitwa *rapid test* ambacho kinatoa majibu kwa dakika chache. Hivyo ndivyo vipimo viwili ambavyo tunavitumia kwa kuchunguza malaria.

Wizara ya Afya ndio inayosimamia malaria na *program* zake, hospitali binafsi nazo zina taratibu zake ambazo hazipo chini ya Wizara ya Afya. Sisi Mnazi Mmoja ndio Hospitali ya Rufaa kwa hiyo ndiyo tunayoiamini, ikiwa hamna tunasema hamna. Sasa hospitali binafsi kama wanafanya mambo yao kwa ajili ya biashara zao hayo mimi siwezi kuyasemea. Ninachojua kwamba vipimo vyetu ni sahihi. Kana anawasi wasi naaje tumuoneshe, tukishachukua kipimo cha damu Mnazi Mmoja, akichukue akapime huko kwengine akatuoneshe hao wadudu wanaowaona wao ambao sisi hatuwaoni.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri naomba niulize swali dogo la nyonge. Pamoja na jitihada za Wizara ya Afya ya Kitengo cha *Malaria Program*, kuonesha jitihada ya kupunguza kasi ya malaria nchini kutoka 9 - 0.7 mwaka 2012. Je, wizara ina mipango gani ya kuhakikisha inatokomeza kabisa masuala ya malaria Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli baada ya jitihada kubwa iliyofanyika Zanzibar ina muelekezo mzuri wa kutokomeza malaria. Hivi sasa bado hajatokomezwa kwa sababu hatujafikia kiwango cha ziro (0). Lakini ili tuweze kufanikisha hilo, mikakati ambayo tumeiandaa ikiwemo ile yote ambayo inatumika ya kutumia vyandarua, yakuwapa wajawazito dawa za malaria, ya kuwapa wagonjwa wanagunduliwa na matatizo ya malaria kuwapa matibabu na upulizaji wa madawa ndani ya majumba.

Lakini kama hiyo haitoshi sasa hivi tunajiandaa, siwezi nikakwambia kwa uhakika kwa sababu hatujalipitisha hilo isipokuwa lipo katika maandalizi, kutengeneza mfuko maalum kwa ajili ya malaria ili kuhakikisha tafiti zinaendelea mpaka tutakapohakikisha malaria imetokomezwa. Kwa hiyo hilo lipo kwenye *process*, halijakamilika kusema sasa kwamba tayari tunafaya kazi, lakini bado *program* ya malaria inaendelea, bado *Global Fund* inafadhili bado PMI inafadhili na serikali inachangia kwa ajili ya hilo, kwa hiyo tunaendelea na kazi.

Nam. 101

Mradi wa Maji Kutoka Japan

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Nafasi za Wanawake): Aliuliza:-
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Sita, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan ilianzisha mradi mkubwa wa maji ili kumaliza tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Hata hivyo, bado wananchi wa Mkoa huo wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji.

(a) Kwa kuwa mradi huo ni mkubwa na Serikali imetumia fedha nyingi; Je, ina mpango gani wa kumalizia mradi huo ili wananchi wafaidike na huduma safi na salama.
(b) Je, kwa hatua iliyofikia sasa, Mradi umegharimu kiasi gani cha fedha.
(c) Hivi ni asilimia ngapi ya wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanapata maji safi na salama.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 101 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mradi wa Maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi umekamilika tangu mwaka 2009, lakini kwa bahati mbaya mradi huo haukuwa wa mafanikio makubwa kwa baadhi ya maeneo, hata hivyo wizara yangu kupitia mamlaka ya maji ina mpango wa kuchimba visima tisa ili kuongeza wingi wa maji katika Mkoa huo na hadi sasa tayari imeshachimba visima vitano. Maeneo ya Chumbuni visima vitatu na Saateni visima viwili. Jitihada za kuchimba visima vyengine vinne zitakamilika mara tu hali ya fedha itakaporuhusu.

b) Mhe. Spika, mradi wa Mkoa wa Mjini Magharibi uliofadhiliwa na serikali ya Japan hadi kukamilika kwake umegharimu jumla ya shillingi za Kitanzania billioni thelathini na mbili na millioni mia Tano (T. Shs. 32,500,000,000.00) ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichangia jumla ya Shillingi

za Kitanzania Millioni Mia Tano (T. Shs. 500,000,000.00) na Serikali ya Japan ilichagia Shillingi za Kitanzania billioni thelathini na mbili (T.Shs. 32,000,000,000.00).

c) Mhe. Spika, wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi hadi sasa wanapata maji safi na salama kwa asilimia 52, hata hivyo Wizara yangu bado haijaridhishwa, na kiwango hicho na ndio maana inaongeza kuchimba visima ili kupunguza tatizo la mgao wa maji uliopo, ili hatimae kuondosha kabisa tatizo la maji hapa visiwani (Unguja na Pemba).

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

(a) Mhe. Waziri kwa vile mradi huu wa maji umeanza kutafuta maji kwa muda mrefu. Je, ni Mikoa mingapi ambayo hivi sasa imeweza kujitosheleza kwa maji.

(b) Ni Mkoa gani ambao unaoongoza kujitosheleza kwa maji hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa taarifa ni kwamba hakuna Mkoa hata mmoja unaojitosheleza kwa maji.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba anijibu swali langu kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama kuna mradi ambao serikali na wafadhili wametumia fedha nyingi hapa Zanzibar ni mradi huu wa maji, lakini inaonekana kwamba kwa serikali ni jambo dogo sana, hatuwezi kutumia zaidi ya bilioni 500 tena bila ya kupata maji kwa wananchi wetu. Hebu atwambie Waziri na wataalamu wake kuna uchunguzi gani uliofanywa wa kina ili Wazanzibari wakatumia mabilioni ya pesa lakini leo hakuna maji hata ya kunawia uso kuna sababu gani za msingi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, suala la kupungua kwa maji ardhini ni kubwa sana na wala si mchezo. Itabidi muda si mrefu tukafanye *desalination* wa kuyatengeneza maji ya chumvi ili tuweze kuyanywa kwa sababu tabia ya nchi imepunguza viwango vya mvua, maji, chini ardhini ni kidogo, kwa hivyo mkifanya uchunguzi leo mtaona maji yapo, mkiweka pampo baada ya muda pampo inanin'ginia hiyo ndio hali hali kwamba maji yameshamalizika. Hili ndio tatizo letu. Serikali inajitahidi sana kutengeneza miradi mingi tu ili kuweza kuhakikisha kwamba maji yanapatikana ya kutosha lakini bado hatujafika lengo hilo. Tutizame chem chem zetu za Mkoa wa Mjini ambazo zilikuwa zikizalisha lita bilioni tatu za maji hivi sasa zinazalisha lita bilioni moja na nusu. Kuna pengo la lita bilioni moja na nusu ambazo zinahitaji kujazwa. Maji ya lita bilioni moja na nusu ni mengi sana ambayo sasa hivi hatunayo. Tumetegemea huu mradi wa visima 9 tunavyochimba hivi sasa hivi tutapata hizo lita bilioni moja na nusu *Ishallah* Mwenyezi Mungu atujaalie iwe hivyo. Hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali langu la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa vile serikali imeweka mradi mkubwa wa maji na mradi huu utawafaa sana wananchi. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri katika jimbo langu la Matemwe kuna visima vingi vimechimbwa pale na mabomba Kiashangwe yametandikwa mengi. Lakini mabomba haya hayajaleta maji ya kuyanufaisha maji ya kuwanufaisha wananchi wa Matemwe ili wakaenea katika kupata hayo maji.

Je, Mhe. Waziri ana utarabu gani wa kuwafanyia umuhimu wananchi wa Matemwe ili yakaweza kufika maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Mwakilishi wa Matemwe yeyé ndiye anayetakiwa na matumaini ya karibu sana kuliko wawakilishi wa maeneo mengine, ana mradi mkubwa wa UUB upo Kiashangwe tangi linajengwa, visima vinane vinachimbwa kwa sababu ya kupeleka maji katika eneo la Matemwe. Kwa hivyo mradi huu kwa kuwa hivi sasa hifi unaendelea na yeyé akipita anawaona Wachina wameshughulika pale wanafanya kazi hiyo, kwa hivyo ajue si muda mrefu tatizo la maji Matemwe litaondoka.

Mhe. Saleh Nassor Juma (Jimbo la Wawi): Aliuliza:-
Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu, na kwakuwa baadhi ya nchi, zikiwemo hata zile zilizoko Kusini mwa jangwa la sahara, hufanya vyema katika Michezo kama ngumi, riadha na tenis, na hatimae kupata medali katika medani ya Kimataifa.

Je, ni lini SMZ itajikita katika Tasnia ya michezo ya Ngumi na Riadha.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Alijibu:
Nakushukuru Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 3 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, jukumu kubwa la serikali katika michezo ni kuandaa mazingira yatakayorahisisha uchezwaji na uendelezaji wa michezo hapa nchini ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu. Jukumu ambalo linatekelezwa vyema serikali na haijashindwa katika hilo. Ila suala la kuendeleza mpira wa miguu limo mikononi mwa Chama cha Mpira wa miguu na wapenzi wa mchezo huo akiwemo Mhe. Saleh Nassor kama mshabiki na mpenzi wa mpira wa miguu.

Mhe. Spika, kuhusu mchezo wa riadha tayari Chama cha Riadha cha Zanzíbar imejikita katika mchezo wa riadha katika kuendeleza na vijana wetu wamekuwa wakifanya vizuri sana. Kwa mfano, mwanariadha Sara Ramadhan alitokea wa kwanza katika mbio ndefu za kilomita 21.5 zilizofayika Mwanza, Brazil na Zanzíbar; mwanariadha John Laurent Kabele alitokea wa 10 miongoni mwa wendaji mbio 400 kwenye Berlin Maratón na wa 11 katika mashindano ya Zanzíbar Island Run ambayo yalikuwa na washiriki 500.

Aidha mwanariadha Asha Mshamba, Mariam Hassan kuruka viunzi na Makame Ali mita 200 wamechukua nafasi ya kwanza katika mashindano ya riadha ya kitaifa yaliyofanyika Dar-es-Salaam, Pia mwanariadha Nagma Jog amechukua nafasi ya pili katika mbio za kilomita 10 zilizofanyika Dubai, Mwanariadha Ester Geoge amechukua nafasi ya kwanza kwenye mashindano ya mbio ndefu ya kilomita 2i, yaliyofanyika Brazil mwaka jana.

Mhe. Spika, matokeo hayo yameridhisha kwamba mchezo huu unapigahatua nzuri katika nchi yetu. Aidha katika kuandaa mazingira ili mchezo wa riadha uweze kuchezwa vizuri, wizara yangu imeagiza vifaa vingi vya riadha karibu makontena mawili yapo nchini yameshafika kwa ajili ya kuendeleza mchezo huo hapa Zanzibar.

Kuhusu suala la mchezo wa ngumi wizara yangu hairuhusu mchezo huu kuchezwa hapa Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo tu la nyongeza.

(a) Pamoja na kunitupia jukumu mimi na ZFA kwamba tunaweza kuuimarisha mchezo wa mpira wa miguu, lakini juhudi zetu tumefanya lakini na serikali kwa upande wake imetenga kiasi gani katika bajeti yake ili kuendeleza huo mchezo.

(b) Pamoja na kwamba wizara yake anasema hairuhusu mchezo wa ngumi lakini kunavijana wetu ambao wameimarika sana Tanzania katika medali ya kimataifa katika huu mchezo wa ngumzi za mateke *(kick boxing)* akiwemo Babu Ali (Ali Van Dame) pamoja na wale vijana wetu wanaofanya *Martial Art Groups* yaani zile judo na karati wanafanya vizuri nje wanapokwenda kushiriki katika mashindano yale.

Je, nyinyi serikali mmewapa motisha gani katika hili, na kama mtawaachia peke yao hawa akina Ali Van Dame na wengine kwa juhudi zao tu bila ya kuwaunga mkono na serikali hamuoni kama mtawavunja moyo, huku wakiwa wanafanya vizuri kuinadi nchi yetu katika michezo hii ya ngumi za mateke *(kick boxing)* pamoja na *matial art*.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika, kama nilivyosema awali sisi kama Wizara kwa niaba ya serikali, jukumu letu kubwa ni kuandaa mazingira mazuri ambapo wananchi kupitia vyama vyao vya michezo watakuwa na urahisi wa kucheza michezo hiyo.

Chama cha Mpira wa Miguu (ZFA) na vyama vyengine jukumu lao ni kuhakikisha kwamba wanatumia mazingira haya ambayo serikali wameyaweka ili waendeleze mpira wa miguu hapa nchini kwa niaba yao na kwa niaba ya wapenzi wao ambao wanashabikia.

Kuhusu michezo mengine midogo midogo kama ambavyo umeitaja judo na karati, serikali inaitambua michezo hii, imeisajili na inashirikiana nao katika kuiongoza. Hivi juzi tu mimi nilikuwa pamoja na Chama cha Judo cha Zanzibar pale Bwawani kuwapongeza, kuwapa nishani na zawadi kwa namna ambavyo waliweza kushiriki vizuri katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ambao wenyewe Chama cha Judo waliandaa vizuri kabisa na wakatafuta fedha karibu milioni 50 katika kuiandaa. Basi na serikali tukatia mkono wetu kuona kwamba Chama hicho kipo makini na kinafanya kazi vizuri.

Kwa hivyo vyama vyote ambavyo vitakuwa makini vinafanya vizuri serikali kupitia Wizara yangu itahakikisha kwamba inashirikiana nao kuhakikisha kwamba michezo ambayo wameibuni wanaiendeleza kuipa nchi yetu heshma ambayo wao wanaipa.

Kuhusu mchezo wa ngumi kama nilivyosema awali hapa Zanzibar bado tumeamua kwamba si mchezo ambao unastahiki kuchezwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kabla ya kumuuliza swali nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri katika taarifa yake ya kusema kwamba kuna vifaa vya michezo wa riadha ambavyo hivi karibuni wanamichezo hao watafaidika na vifaa hivyo ambavyo vipo Bandarini.

Mhe. Spika, katika kuendeleza michezo, mpira wa miguu, riadha na michezo mengine, Zanzibar imechukua muda mrefu kuandaa michezo ya kimataifa ikiwemo mbio za riadha pamoja na mashindano ya mpira wa miguu kama vile *challenge*. Je, wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo ZFA na vyama vyengine kama vile vya riadha ni lini Zanzibar tutaandaa mashindano ya *challeng*e pamoja na mbio za riadha.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika, ni kweli kwa muda mrefu tumekuwa hatujaanza kuandaa mashindano ya kimataifa. Lakini kama nilivyojibu kwamba wiki iliyopita Zanzibar iliandaa mashindano ya judo Afrika ya Mashariki na Kati na tukijaaliwa mwezi wa Juni mwaka huu Chama cha Riadha kwa kushirikiana na Baraza la Michezo litaandaa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati karibu ya nchi 7 itafanyika hapa Zanzibar katika mchezo wa riadha.

Kwa hivyo asiwe na wasi wasi kwamba pengo hili tumeliona na tumeanza kulichangamkia. Mwezi uliopita tumemaliza Judo na mwezi wa Juni tunakuja na riadha na *inshaallah* tukijaaliwa najua kwamba kiu yake ni kuona tunaandaa mashindano ya *Challenge*. Tunazungumza na waandaaji hawa isipokuwa kuna tatizo kidogo kwamba mashindano haya yanadhaminiwa na kampuni za bia jambo ambalo tunazungumza nao kama kuna uwezekano wa kuyadhamini katika utaratibu mwengine basi tutaandaa mashindano ya *Challenge*. Tumewatuma watu wetu na wanalishughulikia hilo.

Nam. 39

Msaada wa Mchele wa Japan kwa SMZ

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali ya Japan imekuwa ikiisaidia Serikali ya Tanzania mchele kila mwaka, mchele ambao kasma ya Zanzibar inakuwamo, na kwa vile ni msaada ungelitarajiwa kupatiwa wananchi bila ya malipo.

a) Je, msaada huo ulianza kutolewa mwaka gani na kila mwaka Zanzibar ilipata kiasi gani kwa thamani gani.

b) Ni utaratibu upi unaotumika wa kuipa Zanzibar mgao wake na kampuni gani zilipewa tenda ya kuleta mchele huo.

c) Tokea Zanzibar ipatiwe mgao wake katika mchele huo wananchi wa kawaida wa Zanzibar wamefaidika nao vipi.

Mhe.Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:

Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima tukiweza kufika hapa katika Baraza hili tukufu. Mhe. Spika naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 39. Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kuhusiana na mchele wa msaada unaotoka Japan kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu wa usambazaji wa mchele wa msaada unatokana na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Japan ambapo Zanzibar imetakiwa kupata asilimia 10 ya mchele huo kila unapoletwa, na kwa mujibu wa makubaliano hayo fedha zitakazotokana na mauzo ya mchele huo zinatakiwa kuwekwa katika akaunti ya Mfuko wa Misaada ya Chakula unaoendeshwa kwa ushirikiano kati ya Serikali hizo mbili.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nichukue fursa hii kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake kama ifuatavyo:-

a) Msaada wa mchele huo ulianza kutolewa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

Mwaka	**Idadi ya Tani**	**Thamani (Shs)**
2004	8,801.12	3, 013, 184,336/=
2005	7,701.53	778, 260,000/=
2009	12,416.19	6, 691, 916,623/=
2011	17,309.09	12, 602, 195,230.5

b) Utaratibu uliotumika mchele huu kuuzwa kwa njia ya zabuni ni kuipa Zanzibar asilimia 10 ya mgao huo na Kampuni ya Zanzibar Romatic ndio iliyopata tenda hiyo.

c) Zanzibar wamefaidika kwa kupata miradi 2 tu ambayo ndio iliyowanufaisha wananchi wa kawaida, mradi wa usambazaji wa maji vijijini, Donge uliopatiwa jumla ya shilingi 58, 888,750. Mradi wa ujenzi wa ghorofa moja ambayo ina madarasa manne na ofisi nne huko Miwaleni Makunduchi Zanzibar ambao una thamani ya shilingi 19, 519,790.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa lengo la mchele huo kutolewa ni kusaidia watu waliopata janga la njaa, je utaratibu uliotumika kwa kuchukua fedha na kupeleka katika miradi zinazotokana na mchele wa sadaka ni kumfanyia haki mwananchi aliyekuwa na shida hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, mchele huu ulipoletwa si kwa madhumuni ya kugaiwa watu nyumba hadi nyumba. Mheshimiwa mchele huu ulipoletwa uliletwa kwa mujibu wa fedha zinazouzwa mchele huu baada ya kupata taarifa kwamba Zanzibar tayari mchele wenu tayari ushaletwa, kwa hivyo sisi tupeleke wafanyabiashara ununuliwe mchele ule utiwe katika mfuko, mfuko huo wa kuendesha miradi ya jamii ndio makubaliano ya mchele huu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa madhumuni ya mchele huu ni kuuzwa na kuekezwa fedha zake katika mfuko wa kusaidia vile vikundi alivitaja. Nilitaka kujua zile fedha ambazo zilitumika katika kusaidia vikundi amevitaja vikundi viwili katika maelezo yake Mhe. Naibu Waziri hapa kwamba vilisaidiwa.

Sasa zile fedha nyengine ziko wapi na zinasaidiwa katika nyanja ipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ahsante Mhe. Spika, fedha zilizobaki katika matumizi ya miradi hii miwili bado fedha ziko katika hiyo akaunti ya pamoja, na fedha hizo zitatumika kwa sababu sisi tunaandika miradi

na miradi ile tunaipeleka katika *steering committee*. Bado tuna miradi chungunzima ambayo inahitajika kutumiwa kwa fedha hizi na hili bado tumeandika miradi na miradi hiyo tayari imo katika *steering committee*, kwa hivyo miradi hii itakuja kutumika kwa fedha hizo si kama fedha hizo zimewekwa tu.

Nam. 51

Ujenzi wa Vituo vya Kuuzia Karafuu

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:

Katika msimu wa karafuu uliopita kwa makusudi Wizara iliweka vituo vya muda vya ununuzi wa karafuu, na kutokana na manunuzi yalivyojitokeza Wizara ilitoa maelekezo ya kujengwa kituo katika kijiji cha Chanjaani (Mtambwe Kaskazini) na Bwagamoyo (Shehia ya Piki).

(a) Je, azma ile ya ujenzi wa vituo hivyo katika sehemu zilizotajwa (Chanjaani na Bwagamoyo) imefikia wapi.

(b) Kama mpango ule upo, basi utaanza lini.

(c) Ikiwa mpango ule umebadilika ni kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 51 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Biashara Viwanda na Masoko imejiwekea utaratibu wa kuvikarabati vituo vya zamani na kujenga vipya katika maeneo ambayo Serikali itaona inafaa kufanya hivyo kwa azma ya kuwaondoshea usumbufu wakulima wa zao la karafuu la kutembelea masafa marefu ili kwenda kuuza karafuu zao. Aidha Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa makusudi imeamua pia kuvifanya vituo hivyo kuwa ni vivutio kwa wakulima kwa kujenga vyoo na maeneo ya kukaa wakati wa kusubiri uuzaji wa karafuu zao pamoja na kuwapatia huduma za maji ya kunywa.

(a) Katika kutekeleza azma hii nzuri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia Shirika lake la ZSTC tayari imeshaandaa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitano (5) kwa mwaka huu wa Fedha wa 2013/14 vikiwemo hivyo vya Chanjaani na Bwagamoyo. Vituo vyengine ni vya Gando, Chambani na Wambaa.

(b) Mhe. Spika, kama ambavyo nimekwishajibu katika jibu (a) tayari fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vitano (5) ambavyo nimevitaja hapo juu zimeshapangwa na zinatarajiwa kuingizwa katika mpango wa bajeti ya Shirika la ZSTC kwa mwaka wa Fedha unaokuja

(c) Mpango wa ujenzi wa vituo hivyo mpaka sasa bado haujabadilika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, lilitokea suala kama hili na nilipouliza niliambiwa kuwa hakuna mpango wa kujenga vituo hivi lakini vituo vilivyotajwa ni vitatu na ikaongezwa kuwa tunapojibiwa tusikilize kwa makini kauli ambayo sikuifurahia. Na leo tunaambiwa kwamba vituo hivi vitajengwa nataka usahihi kwa sababu ya kauli mbili hizo vitajengwa kweli au ndio ile kauli ya nyuma.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ningependa Mhe. Salim Abdalla Hamad awe anaiamini sana serikali yake ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoendeshwa kwa mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Serikali hii Mhe. Spika, inapojipangia masuala yake na hasa katika Wizara hii ya Biashara, bila shaka utaratibu wa utekelezaji pia unaandaliwa. Mimi ninamwambia kwa niaba ya Wizara kwamba vituo vyake hivyo viwili vya Chanjaani na Bwagamoyo viko katika mpango wa ujenzi kwa mwaka huu wa fedha basi aamini hivyo. Ingelikuwa fedha hakuna Mhe. Spika, ningemwambia fedha hakuna lakini nimemwambia fedha zimeshatengwa na si vituo vyake tu lakini fedha zimetengwa kwa vituo 5, na vituo 5 hivyo *inshaallah* Mwenyezi Mungu atajalia vitajengwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufasaha na tumemuelewa. Lakini napenda nimuulize kwa kuwa yeye amesema kama anategemea kama mwaka huu wa fedha kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu vituo hivyo vitajengwa. Sasa napenda nimuulize ni kiasi gani cha fedha zimetengwa kwa ajili ya kujenga vituo hivyo, na je hivyo vituo vitakavyojengwa vitajengwa kwa tenda au watajenga wananchi wa maeneo ambayo watakuwa wapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimesema kwamba fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo 5 kwa mwaka huu wa fedha 2013/14 zimeshatengwa na ni jumla ya pesa za kitanzania 3, 000,000.

Nam. 31

Upungufu wa Vitendea Kazi Maskulini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Elimu bure likuwa ndiyo sera ya elimu iliyoasisiwa na muasisi wa Mapinduzi Matukufu ya 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiendeleza sera hiyo katika awamu mbali mbali zilizopita. Hata hivyo sera ya elimu bure lazima iende sambamba na elimu bora. Na elimu bora inapatikana tu kama kutakuwa na walimu bora, vitendea kazi vya kutosha kama maabara, madeski, chaki, vitabu, mazingira mazuri ya kujisomea n.k

(a) Je, Serikali ina maelezo gani kuhusu upungufu wa vitendea kazi katika skuli nyingi nchini.

(b) Kwa kuwa walimu bora ndio kichocheo kikubwa cha kupatikana kwa elimu bora, kwa nini Wizara haitoi motisha (*incentives*) kwa walimu wanaofanya vizuri.

(c) Serikali inatathmini vipi ubora wa elimu na mitaala yetu katika kuandaa upatikanaji wa wataalamu wa baadae katika kada mbali mbali nchini kama vile wahandisi, madaktari, walimu, wanasayansi n.k

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 31 lenye sehemu (a) , (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kabla sijamjibu napenda kutoa maelezo ya utangulizi machache na nitaomba nizungumze pole pole kwa utulivu ili Mhe. Jaku pamoja na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu walielewe hili suala ambalo nitalijibu kwa sababu ni suala muhimu.

Mhe. Spika, hivi karibuni Baraza la Mitihani NECTA ni kweli lilitoa taarifa kwamba wanafunzi wa form Six mwaka huu wataruhusiwa kufanya mitihani baada ya kuonekana wamefaulu masomo 5 kati ya hayo matatu kwa kiwango cha *credit* yaani C na mawili kwa kiwango cha pasi ya kawaida. Tangazo hilo limetolewa lakini tangazo limetolewa bila ya maafikiano au makubaliano au mazungumzo kati ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuwa tunajua NECTA ni chombo cha Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo swali (a) napenda kulijibu kama ifuatavyo:-

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Jaku ameuliza je kuna ukweli wa suala hilo kama Zanzibar iliarifiwa.

Nasema hakuna ukweli wa suala hilo, Zanzibar kama ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya amali inawakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuarifiwa na isingepaswa kuarifiwa ingepaswa kushirikishwa katika kujadili swali hilo.

Kwa sababu hiyo Zanzibar kwa suala la (a) kwa ufupi nasema Zanzibar haikuarifiwa.

b) Anauliza Wizara ya Elimu Zanzibar haioni kuwa inachelewa kuwaweka wanafunzi wake katika mazingira mazuri ya mabadiliko hayo ili kuweza kufaulu vizuri mitihani yao.

Mhe. Spika, nasema hatukuwa na haja ya kuwaweka wanafunzi wetu katika mazingira mazuri ya kufanya mitihani yao kwa aina na utaratibu ambao hatukujadili na tukakubaliana. Kwa hivyo sisi tuliona wanafunzi wetu wabakie kama walivyo kwa kufuata utaratibu ule ule tunaouelewa.

Mhe. Spika, tulitoka sisi Wizara ya Elimu nikiongoza ujumbe kwenda Tanzania Bara Wizara ya Elimu ili kuzungumza na Waziri wa Elimu kwa sababu hoja iliyokuja ni kwamba NECTA inafuata maagizo ya Wizara ya Elimu na Ufundi ya Tanzania Bara. Tulikwenda huko kuzungumza na wenzetu kujua ukweli wa jambo hili. Bahati nzuri Waziri wa Elimu na Ufundi wa Tanzania Bara alikuwepo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo alikuwepo, na Kamishna anayeshughulikia NECTA alikuwepo.

Baada ya kutoa hoja hii kwamba mabadiliko haya mbona mmeamua peke yenu hatukuelewana, hatukulizungumza hatukukubaliana Waziri wa Elimu aliwauliza Maofisa wake hili mnalijua, hakuna aliyejibu kwamba wanalijua. Kwa hivyo inaonekana lilikuwa la kushtukiza na la uzushi sio la uhakika.

Waziri wa Elimu alinigeukia akanambia Waziri unataka tufanye nini? Nikamueleza la kwanza tunataka wanafunzi wetu wote waruhusiwe kufanya mtihani kwa utaratibu ule ule waliouzoea na kwa viwango vile vile walivyopasia.

La pili wanafunzi wetu wa mwaka ujao yaani mwaka huu wa 2013/14 waruhusiwe pia kufanya mitihani yao kwa utaratibu huo huo tuliokubaliana sio huu mpya.

Na la tatu nataka tukubaliane kwamba tukutane mara kwa mara na tuamue kwa pamoja kabla suala hili hatujaliamua. Waziri wa Elimu alikubali na akatoa agizo kwa maofisa wake wawili waliokuwepo pale rudini mkatekeleze hilo.

Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu wanafunzi wetu wa mwaka huu wa Tanzania nzima walifanya mtihani kwa utaratibu ule ule tuliokubaliana mapema sio utaratibu huu mpya uliozuliwa kwa ghafla.

c) Wizara itawasaidia vipi wanafunzi ambao hawajatimiza sifa za kuwa na alama hizo 5.

Mhe. Spika, Wizara haikuwa na haja kufanya hivyo kama nilivyokwisha kueleza na mitihani wanafunzi wetu wote waliruhusiwa kufanya, wameshafanya na mitihani imeshakwisha tunasubiri matokeo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa zamani kwa kuweka uwazi kabisa suali hili Mhe. Shamuhuna nikushukuru sana kabisa kwa kutuelimisha na kutupa darasa muda huu. Baada ya hayo nikuulize maswali 3 tu madogo ya nyongeza.

Kiwango cha alama za kufanya mtihani wa kitaifa mwanafunzi anatakiwa awe ana alama ngapi.

Baada ya mazungumzo ya Wizara mbili je, wanafunzi wa Zanzibar wataendelea kutumia alama zile za zamani au utaendelea kudumu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, tunakubaliana kwa utaratibu uliopo wanafunzi wanaofanya mitihani ya *form six* ni wale ambao wana matokeo ya C tatu na nyengine za aina yoyote ikiwa ni B, ikiwa ni C ikiwa D *what ever* lakini na alama nyengine walizopasi. Hayo ndio makubaliano yetu ya zamani na ndio tunayoendelea nayo na ndio yanayotumika kufanya mitihani safari hii.

Lakini swali la (b) ninamuomba kidogo alirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, baada ya mazungumzo ya Wizara 2 nasema wanafunzi wataendelea kutumia alama ile ya zamani au ishakuwa ya muda wa moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nilisema nitazungumza pole pole na kwa uwazi ili nifahamike, inaonekana Mheshimiwa labda hakulisikia jibu langu nilipotoa jibu la msingi. Nilisema wanafunzi wa mwaka huu wameshafanya huo mtihani kwa kutumia alama zile zile za zamani sio mpya, na wa mwakani vile vile watafanya mitihani yao kwa kutumia alama zile zile mpaka hapo tutapokutana sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano kuizungumza suala hili na kukubaliana ndipo marekebisho na mabadiliko ya alama za kupasisha wanafunzi kufanya mitihani yatakapokubalika.

Nam. 20

Mgawanyo wa Madaraka na Haki za Binaadamu

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu
Na kuweka utekelezaji wa majukumu na uwezo na
Mambo yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba mswada wa kuanzisha Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu sasa usomwe kwa mara ya Pili.

Mhe. Spika, naomba pia kutoa hoja kuwa mswada huu usomwe pamoja na marekebisho yake yaliyogaiwa chini ya kifungu cha 84(2)(a) ya Kanuni za Baraza. Mhe. Spika, marekebisho haya ni yale yote ambayo Kamati ya Katiba na Sheria iliyapendekeza na Wizara yangu ikayakubali mapendekezo hayo yote.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara na kwa niaba yangu binafsi naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Katiba na Sheria kwa juhudi zao walizozichukua pamoja na ushirikiano wao waliouonesha. Si kwa mswada huu tu lakini kwa mambo yote waliyotuelekeza kuanzia 2010.

Mhe. Spika, marekebisho yaliyofanywa yamesaidia sana sana kuweka mswada huu wetu katika hali nzuri zaidi. Marekebisho kama yalivyopendekezwa na Kamati ni ya kifungu 2,3 Kifungu cha 3 kifungu cha 4(1) kifungu cha 11(1) kifungu cha 15, kifungu cha 16, kifungu cha 24 na kifungu cha 26(1). Marekebisho yote hayo tumeyakubali na kwamba yale maoni yote yaliyotolewa na semina ndogo ya Wajumbe ambayo tuliifanya hivi karibuni tumeyazingatia na tumeyaweka katika marekebisho hayo ya mswada huo.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya mswada huu ni kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kuweka utekelezaji wa majukumu na uwezo wa mambo yanayohusiana na hayo. Wadhifa wa Mwanasheria Mkuu umeanzishwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa mujibu wa katiba, Mwanasheria Mkuu ni mshauri mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kazi zake nyengine zimeelezewa na sheria zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, kuna mapungufu mengi ya kimsingi ambayao yanaathiri ufanisi wa ofisi, njia pekee ya kuondosha mapungufu hayo ni kwa kutungwa sheria hii ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar sheria ambayo imeweka kisheria kuanzishwa kazi mbali mbali ambazo zitashughulikiwa na Mwanasheria Mkuu na Wasaidizi wake.

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo ambayo yanaathiri utendaji ni pamoja na mambo yanayofuata:

1. Mwanasheria Mkuu hana uhakika wa kuwa na msaidizi mkuu, kwa maana hiyo sheria hii imetekeleza suala hilo.
2. Baadhi ya kazi, majukumu na uwezo unaotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu haujaelezwa waziwazi katika sheria bali zinatekelezwa kutokana na uasili wa ofisi yenyewe tu na mazoea (*convention* tu).

3. Hakuna miongozo inayoongoza namna ya kushughulikia mambo muhimu kama vile usimamizi wa kesi, uandishi wa hati za kisheria na kadhalika.
4. Hakuna namna nzuri ya kulinda maslahi ya serikali katika makubaliano ya kibiashara yakiwemo mikataba ya biashara ya serikali na hati za maelewano, taasisi za serikali na kadhalika.
5. Muundo uliopo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hauendani ya ufanisi, hakuna mgawanyo wa vitengo, wakili yeyote wa serikali anaidhinishwa kufanya kazi yoyote hali inayopelekea ugumu katika kutambua vipaji vyao na kuviendeleza ipasavyo.
6. Hakuna sheria inayoelezea hadhi ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na chombo kinachoweza kutengua ushauri huo. Hili ni tatizo kubwa na katika mswada huu limerekebishwa.

Mhe. Spika, mbali na mambo hayo mengine wanasheria kwa mfano wanafanya kazi katika taasisi tofauti wakati kazi zao zina mahusiano ya moja kwa moja na kazi za Mwanasheria Mkuu na utekelezaji wa kazi zao una athari ya moja kwa moja kwa serikali na jamii, lakini Mwanasheria Mkuu hajapewa wajibu wa kukuza fani ya sheria, ujuzi na uwezo wa mawakili wetu, maafisa wa sheria na makarani wa sheria.

Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika sehemu tano na una vifungu 32. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya awali, inaelezea jina fupi na kuanzisha kutumika matumizi na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika.

Sehemu ya pili inahusu uanzishwaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, watendaji wa ofisi, sifa zao na bajeti za fedha za ofisi, hii ina vifungu kuanzia cha nne mpaka cha 24.
Mhe. Spika, kifungu cha tisa mfano kinahusu ajira ya watumishi wa kitaalamu na wasaidizi ambao utafanyika kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma. Kifungu cha kumi kinatoa masharti ya uajiri wa wanasheria wa afisi. Kifungu hiki kinatoa masharti kwa Mwanasheia atakaeajiriwa katika Ofisi ya Mwansheria Mkuu ataanza ajira yake kama afisa wa sheria na atakuwa wakili wa serikali na kupangiwa kazi za wakili wa serikali iwapo baada ya kufanya kazi atatimiza sifa za kuwa wakili wa serikali.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu inahusu udhibiti na utendaji kazi na utekelezaji majukumu ya ofisi. Sehemu hii ina vifungu kumi kuanzia kifungu cha 14 hadi cha 24. Kazi hizo Mhe. Spika, ambazo zimeelezwa katika kifungu cha 14 ni pamoja na kuwezesha utekelezaji wa kazi na uwezo aliopewa Mwanasheria Mkuu kama ilivyoelezwa katika katiba na sheria nyengine husika, kuanzisha na kuifanyia mapitio sera na taarifa zinazohusiana na waandishi wa sheria na waandishi wa hati zisizokuwa za kisheria, kutayarisha na kusimamia taratibu zote za utayarishaji miswada, sheria, kanuni na hati nyengine za kisheria na kuwezesha kuchapishwa katika gazeti na kutoa ushauri wa kisheria kwa serikali na jambo lolote la kisheria na kutoa ushauri kwa serikali na taasisi za umma katika kupatana na kutayarisha mikataba ya kibiashara na mikataba mwengineyo.

Mhe. Spika, kifungu cha 15 kinatoa haki kwa Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya kufanya shughuli za kisheria na haki ya kusikilizwa katika vyombo vya kimahakama ambapo pia inampa haki Mwanasheria Mkuu iwapo si sehemu ya kesi ya madai kuomba kusikilizwa katika kesi hiyo yaani kwa kuingizwa pamoja.

Mhe. Spika, vifungu hivi vinaendelea mpaka katika kifungu cha 24 ambapo kinaelezea utaratibu mzima wa shughuli za Mwanasheria Mkuu.

Katika sehemu ya nne Mhe. Spika, inaelezea kanuni za maadili kwa mawakili wa serikali na maafisa wa sheria. Sehemu hii ina vifungu vya 25 mpaka 27. Kifungu cha 25 kinampa uwezo Mwanasheria Mkuu kutunga na kusimamia kanuni za maadili kwa mawakili wa serikali na maafisa wengine wa sheria. Wakati kifungu cha 26 kinaruhusu kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu mtu anayekiuka kanuni na maadili hayo. Kifungu cha 27 kinampa wajibu Mwanasheria Mkuu kwa kuweka viwango vya utendaji vya kuzingatiwa na kufikiwa katika kila kitengo cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu au idara au kitengo cha sheria cha taasisi ya umma inayohusika na masharti ya sheria hii.
Sehemu ya tano Mhe. Spika, inahusu masharti ya jumla, ina vifungu 28, 29, 30, 31 na 32. Kifungu cha 28 kinatoa kinga kwa kitendo au kitu chochote kilichofanywa na kuachwa kufanywa kwa nia safi na Mwansheria Mkuu, naye Mwanasheria Mkuu pamoja na Mawakili wa Serikali na Ofisa wa Sheria. Kifungu cha 29 kinatoa masharti ya mashirikiano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, mashirikiano haya Mhe. Spika, ni pamoja na kubadilishana ujuzi ambao ofisi mbili hizi unazo.

Mhe. Spika, utaona kwamba ofisi ya Mwendesha Mashtaka ni ofisi ambayo inahusiana sana na kesi za jinai wakti Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inahusiana sana na masuala ya *civil* pamoja na mikataba. Kwa hivyo, wanasheria hawa wanapopata nafasi ya kubadilishana ujuzi inaweza ikasaidia sana katika mfumo mzima wa wanasheria wetu kukuza ujuzi kwa sababu wote hawa ni watendaji wakuu wa serikali.

Kifungu cha 30 kinampa haki Mwansheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu kuwa ni wachukuaji wa viapo wakati kifungu cha 31 kinampa waziri kwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii.

Mhe. Spika, kifungu cha 32 ambacho ni cha mwisho kinapambanua kuhusu Naibu Mwanasheria Mkuu aliyepo na Mawakili wa Serikali waliopo na kwamba itapoanza kazi sheria hii kutokana na kifungu hiki basi hao wataendelea kuwa ni maofisa wanaotambulika kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu na Maofisa wa Sheria kama walivyo hivi sasa. Kwa hivyo, kifungu hiki ni muhimu Mhe. Spika, kwa kuwatambua watendaji hawa baada ya sheria hii kupita.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba Waheshimiwa Wajumbe waujadili mswada huu ili waweze kuelekeza na hatimaye waupitishe ili iweze kuwa sheria ambayo itasaidia sana katika utendaji wa shughuli zetu za serikali. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny. Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kunipa nguvu za kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, halikadhalika napenda kukushukuru na wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya awali kutoa maoni ya Kamati juu ya Mswada huu ambao ni muhimu katika kuimarisha utawala bora katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Kamati yangu inawapongeza sana Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, wakiongozwa na Mwanasheria Mkuu, na wale wote waliohusika kwa namna moja au nyengine, katika kutayarisha Mswada wa Sheria hii.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012, kifungu cha 83 (5) ambacho kinasomeka kama ifuatavyo:
“Kamati iliyopelekewa mswada kwa mujibu wa kanuni hii inaweza kumualika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya kamati hiyo, kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wake kwa mswada unaohusika”

Kwa ujumla vifungu hivi vinatoa fursa ya kuwaalika wadau wa sekta husika katika kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada husika, Kamati ilifanya hivyo kama Kanuni ilivyoelekeza ambapo wadau wa sekta ya Sheria walifika na kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada huu. Kwa msingi huo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa wadau wote walioshiriki kutoa maoni yao ambayo yameisaidia sana Kamati katika kufanya marekebisho haya, mawazo ya wadau hao yanaheshimwa sana na tunapenda kuchukua nafasi hii kuwaeleza wadau wote kuwa wasichoke kutusaidia pale tunapohitaji msaada wao.

Mhe. Spika, nitakuwa mpungufu wa fadhila nisipowapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wote ambao Kamati ikifanya kazi za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuihoji serikali na kutoa, maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika serikali.

Mhe. Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ali Abdalla Ali - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - MakamoMwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Mjumbe
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe

7. Mhe. Mohammedraza H. Mohammedali - Mjumbe
8. Ndg. Latifa Saleh Suleiman. - Katibu
9. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswaada huo uliokuepo juu ya meza hivi sasa kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kusema kwamba kitendo cha Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuamua kuandaa Mswaada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni jambo la kupongezwa hasa ukizingalia hapo awali walikua wakifanya kazi zao bila ya kuwa na Sheria, kitendo ambacho kilisababisha mapungufu mengi katika utendaji wa kazi zao. Hivyo Sheria hii ndio itakayokua mkombozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo italeta ufanisi katika majukumu yao ya kuishauri Serikali kama wadhifa wa Mwanasheria Mkuu unavoelezewa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu umetungwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba, kazi zote zinazohusiana na mambo ya Kisheria zitakua chini ya usimamizi maalumu kwani hapo awali tunaona kwamba kazi hizo zilifanywa bila ya kuwa na msimamizi rasmim hali ambayo ilipelekea kuwa na mkanganyiko wa majukumu. Hivyo Sheria hii imekuja kuweka misingi imara ya utendaji na uwajibikaji.

Kamati imefurahishwa sana kuona kuwa katika Mswada huu umeainisha mfumo mzima wa kupatikana Naibu Mwanasheria Mkuu ambae atakua ndie msaidizi wa Mwanasheria Mkuu katika mambo yanayohusiana na utendaji kazi na pia Mswada umeelekeza taratibu za kupatikana kwake. Mhe. Spika jambo hili linadhihirisha kwamba nchi yetu imefikia katika viwango vya kimataifa vya haki, uwazi na ukweli, hivyo kuna haja ya kuitumia nafasi hii kwa umakini zaidi.

Mhe. Spika, tunaunga mkono vifungu mbali mbali vilivyopo katika Sehemu ya tano ya Msawada huu. Hii ni kutokana na kuwa Mswada umeeleza mashirikiano yatakayokuwepo baina ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwani Taasisi hizi mbili ndio nguzo mama ya Nchi kwa upande wa utowaji haki kisheria. Mhe. Spika Kamati pia imefarajika sana kwavile Mswada huu wa Sheria utaleta tija kwa watumishi wote wa Umma ambao wameajiriwa kutoa huduma za kisheria, kwani kutakua na fursa kwa Watumishi hao kupata taaluma na mbinu mpya na za kisasa katika utendaji wa kazi zao za kila siku.

Mhe. Spika, suala la nidhamu ni kitu cha msingi katika ufanisi na utendaji kazi kwa taaluma ya Kisheria kwani wao ndio muongozo katika kuleta misingi ya haki na usawa kazini. Mhe. Spika mambo mengi ya ukiukwaji wa maadili kazini yanajitokeza kwavile hapakuwepo na msimamizi wa watu wenye fani hizo za Sheria.
Mhe. Spika, tunaimani kuwa pindi itakapoanza kazi Sheria hii, utendaji kazi wa pamoja utapatikana kwani kabla ya kuwepo kwa Sheria hii tunaona kuwa Taasisi za Serikali zilikua zikiingia katika Mikataba na makubaliano na Taasisi nyengine bila hata kuzingatia ushauri wa kisheria kutoka katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu na hatimae mikataba hiyo hua haileti tija na kusababisha hasara kwa serikali na wananchi kwa ujumla ambao ndio walipa kodi wa nchi hii.

Mhe. Spika, baada ya kuupitia Mswada huo, Kamati yetu imependekeza kufanyiwa marekebisho kwa baadhi ya vifungu kwa lengo la kusaidia kuimarisha Mswada huo wa Sheria. Mfano wa vifungu hivyo ni kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 3, tafsiri ya neno Afisa wa Sheria, isomeke," ni mtu mwenye shahada ya sheria inayotambulika aliyeajiriwa katika utumishi wa umma kutoa huduma za sheria isipokuwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahakama na Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Spika, Kamati imependekeza pia Kifungu cha 11, yaongezwe maneno "Kwa kushauriana na Mkuu wa taasisi au mamlaka husika" baina ya maneno "Mwanasheria Mkuu" na "anaweza". Na kifungu kisomeke, "Bila ya kujali sharti la kifungu cha 12, Mwanasheria Mkuu kwa kushauriana na Mkuu wa taasisi husika anaweza kumteua Afisa wa Sheria yeyote kutoka ofisi yoyote ya Utumishi wa Umma kuwa Wakili wa Serikali kufanya kazi maalum au za jumla za Mwanasheria Mkuu kama itakavyoainishwa katika barua ya uteuzi. Katika sehemu ya tatu kifungu cha 16(j), yaongezeke maneno "kwa mujibu wa sheria" baada ya maneno "Utumishi wa Umma".

Mhe. Spika, kimsingi huu ndio muhtasari wa Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na mengine yataonekana katika waraka wa marekebisho uliowasilishwa mbele ya Baraza hili. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie Mswada huu kwa madhumuni ya kuuimarisha zaidi na hatimae kuukubali kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa wenzangu hawajajipanga vizuri basi naona nitumie fursa hii kusema mawili matatu ili kutoa nafasi kwa wenzangu kuweza kujipanga vizuri na hatimaye kuchangia mswada huu.

Mhe. Spika, Mswada huu ni mzuri na ni muhimu kuupitisha ili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na watendaji wake basi wawe sasa wanasimamiwa na sheria kuliko hivyo ilivyokuwa kabla.

Mhe. Spika, katika kuusoma Mswada huu nimegundua jambo moja muhimu sana na ni kwamba unaanzisha mtandao wa nchi nzima wa wanasheria ambao watakuwa wanasimamiwa na ofisi moja, kwa maana hiyo basi kutakuwa na maelekezo ya aina moja, kutakuwa na maadili ya aina moja na pengine kutakuwa na *uniformity* hata ya maslahi ya wanasheria.

Mhe. Spika, mfumo kama huu pia uko kwa wale Wahasibu wa Serikali, pia wanakuwa *control* na ofisi moja. Sasa hili nadhani ni jambo zuri na linaweza likaweka nidhamu nzuri zaidi ya wanasheria wetu. Kwa hivyo, labda nianze kwenye kifungu cha tano.

Mhe. Spika, katika kifungu cha tano ndipo alipotajwa Mwanasheria Mkuu, lakini hapa maoni yangu Mhe. Spika, ukisoma kifungu hiki basi hakianzishi Mwansheria Mkuu kimetaja tu kwamba Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye mkuu wa ofisi lakini hakianzishi Mwanasheria Mkuu. Nilikuwa nadhani ni vyema pamoja na kwamba Katiba ndio inasema Mwanasheria Mkuu, lakini hiki kifungu kingetaja basi kinaanzisha Mwanasheia Mkuu pengine na sifa zake na majukumu yake yamo yameelezwa humu ndani lakini angalau kianzishe. Kwa hivyo, nilikuwa naona Waziri hapa afanye marekebisho ili sheria hii nayo pia ianzishe hasa huyo Mwanasheria Mkuu kama ambavyo kifungu cha sita kinaanzisha Naibu Mwanasheria Mkuu, hiki kinaanzisha hasa kwamba kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu ambaye atateuliwa na Rais, lakini hiki kifungu cha tano hakijataja mambohaya.

Jambo jengine ambalo nilidhania niliseme kidogo Mhe. Spika, ukisoma kifungu cha 6(2) kimeeleza sifa za mtu atakayekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu. Kwa mawazo yangu Naibu Mwanasheria Mkuu ni mtu mkubwa sasa asingepaswa kulingana na Afisa wa Sheria, lakini sasa ukisoma hapa katika sifa zake imeelezwa pale kwanza (a) awe ni Mzanzibari sawa, lakini (b) ana elimu isiopungua shahada ya kwanza ya sheria kutoka Taasisi ya Elimu ya Juu inayotambulika na chombo chenye mamlaka. Sasa sifa hii anayo yule Afisa wa Sheria ambaye kwa cheo atakuwa Afisa wa Sheria ni mdogo kuliko Naibu Mwanasheria Mkuu, sasa nilikuwa nadhani si vibaya pengine sheria ingetaja mwenye elimu ya juu zaidi kuliko yule Afisa wa Sheria pengine awe na *master degree* ya sheria au vyenginevyo, lakini ukimuweka sawasawa utakuja kukuta siku moja hata ile kuwekeana nidhamu kunaweza kuwa kudogo.

Mhe. Spika, labda nikiondoka hapo niende kwenye kifungu cha 7(2) kinasomeka hivi, “isipokuwa kama Rais ataamua vyenginevyo pale ambapo Mwanasheria Mkuu hawezi kutekeleza wajibu wake kwa muda kwa sababu ya kutokuwepo ofisini, ugonjwa au sababu nyenginezo”. Sasa tatizo langu lipo pale Mwanasheria Mkuu hawezi kutekeleza wajibu wake kwa muda haukuelezwa ni kwa muda gani, pengine amekusudia ni kwa muda mrefu lakini imeandikwa hivyo tu kwa muda. Sasa nilikuwa napendekeza pale ule muda uainishwe basi kama ni miezi mitatu au sita au vyenginevyo, lakini isiwekwe hii kwa muda maana yake inakuwa haitoi tafsiri halisi. Nadhani itakuwa imeeleweka hiyo.

Sasa Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 10(2) kuna neno sikulipenda nafikiri ni *translation*, kinasema kwamba, “Mwanasheria Mkuu anaweza kuwa *notice* itayochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kumteuwa Afisa yeyote wa Sheria aliyeajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa wakili wa serikali na kumpangia kazi za wakili wa serikali iwapo ataridhika kwamba amepata uzoefu na uelekevu”, sasa tatizo langu ni hili neno ‘uelekevu’ Mhe. Spika halijanikalia vizuri. Nadhani tungetafuta lugha nyengine hapa au itoshe hii kwamba amepata uzoefu wa

kutosha unaohitajika kuwa wakili wa serikali, hili neno uelekevu mimi silipendi sana kwa Kiswahili chetu sanifu halielekei vizuri.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye kifungu cha 14. Unajua Mhe. Spika, tumekuwa tukipata tabu sana katika utendaji wetu wa taasisi za serikali hasa pale tunapoingia mikataba ama na taasisi za nje au hata wahandisi au vyenginevyo, mara nyingi mikataba yetu inakuwa haiko kwenye viwango vinavyotakiwa na matokeo yake utekelezaji wa shughuli iliyokusudiwa huwa ngumu, na mara nyengine huwa ni hasara kwa serikali.

Sasa nimefurahishwa sana na kifungu hiki cha 14 hasa ukiangalia kwenye kifungu hiki cha (h) na (l), kwamba Mwanasheria Mkuu miongoni mwa kazi zake ni kutoa ushauri wa kisheria, yaani yeye au wale maafisa wake ambao watakuwa wamechawanywa kila taasisi kutoa ushauri wa kisheria kwa serikali na taasisi za umma katika kupatana na kutayarisha mikataba ya kibiashara na mingineyo isiyokuwa ya kibiashara kwa niaba ya serikali. Yaani ile mikataba ikipata Baraka za Mwanasheria Mkuu na wale watendaji wake wanasheria aliowachawanya katika taasisi za serikali basi huenda taasisi zile zikawa makini katika kuingia mikataba. Lakini si vibaya vile vile kuwa na mfumo maalum ambao utakuwa unajulikana kwamba kwa mkataba wa ujenzi basi kuwe na *item* hii na hii yaani kuwe kama na *formula* ya kuingia kwenye ule mkataba.

Mhe. Spika, mikataba mengine kuna mambo muhimu sana huyakuti mule na ndio yanayosababisha matatizo mengi. Kwa hivyo mfumo huu nadhani kwa usimamizi huu huenda sasa taasisi zetu za serikali zikawa zinafanya mikataba iliyo makini ambayo italipa maslahi ya serikali na kuepushia kupata hasara za kila siku zisizokuwa za lazima.

Kwa hivyo hapa napongeza. Nafikiri Mhe. Spika, kama nilivyosema awali huyu mswada ni mzuri sana na kwa kweli ukiangalia hata sababu za kuletwa huu mswada ni nyingi na za maana sana. Mimi binafsi sina tatizo nao na nauunga mkono sana kwa asilimia mia moja. Baada ya kusema hayo naomba nikae kitako.

Mhe. Spika: Majadiliano yanaendelea, naona kama Mhe. Fatma anataka kusema hivi karibu, imekuwa kukamatia kamatia hivi, hajajitayarisha bado.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii angalau kuchangia mawili matatu kwa sababu mswada huu kwa kweli ni mkubwa na ikisha ina uzito wake kwa kiasi Fulani.

Kwanza nimshukuru waziri kwa kuwasilisha mswada huu na vile vile niishukuru kamati kwa kutoa maoni yake na pia niwapongeze wadau waliochangia mswada huu. Ni kweli kwamba hivi sasa serikali imekomaa kiutawala; haki na uwazi katika serikali inaonesha kwamba kuna ufanisi katika kusimamia mambo yake.

Mhe. Spika, nikenda kwenye madhumuni ya mswada huu kwa kweli madhumuni yake ni makubwa ya kumpa Mwanasheria Mkuu Kikatiba kuwa mshauri mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kazi zake nyengine zimeelezwa na sheria hii ambazo zitatungwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu ni muhimu sana na umekuja kwa wakati muafaka. Mhe. Spika, nikenda katika madhumuni haya nitoe msisitizo kwa madhumuni ambayo yamesema hakuna namna nzuri ya kulinda maslahi ya serikali makubaliano ya kibiashara, ikiwemo mikataba ya kibiashara ya serikali na hati za maelewano.

Taasisi za serikali zinaweza kutumia mikataba maalum inayotumiwa na taasisi zinazotambulika katika kila fani ya mapatano ya kibiashara ambazo zinaweza kuhatarisha maslahi ya serikali. Mhe. Spika, kuhusu hili jambo la mikataba kwa sababu kumejitokeza mikataba mingi ambayo inakuwa mikataba ni mibovu kutokana na hali ya uharaka basi tukatiliana saini mikataba ambayo si mizuri. Kwa hivyo Mwanasheria ni mmoja ambaye atakuwa na nguvu sasa kuisimamia mikataba hii.
Vile vile nikenda kwenye hayo hayo madhumuni ukurasa nambari 333, naomba Mhe. Spika, uniruhusi ninukuu *paragraph* ya tatu inayosema “Mwanasheria wanafanya kazi katika taasisi kuna ofauti ni tofauti, sijatizama kwenye marekebisho lakini nafikiria ni tofauti wakati kazi zao zina mahusiano ya moja kwa moja na kazi ya Mwanasheria Mkuu.

Wanasheria wanafanya kazi katika taasisi tofauti wakati kazi zao zina mahusiano ya moja kwa moja na kazi za Mwanasheria Mkuu, na utekelezaji wa kazi zao unaathari ya moja kwa moja kwa sheria na jamii. Lakini Mwanasheria Mkuu hajapewa wajibu wa kuhakikisha kukuza fani ya sheria, ujuzi na uwezo wa mawakili wa

serikali, maafisa wa sheria na makarani wa sheria. Mimi ninasema hapa Mhe. Spika, ni lazima kuwe na *network* ya hawa wanasheria wa taasisi mbalimbali pamoja na Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, vile vile nikirudi ninakwenda mbele halafu ninarudi nyuma ukurasa huu wa 320 unasema kwamba *paragraph* kwenye kitoto cha tatu "muundo wa ofisi", kwenye kifungu nambari 8 (3) "Iwapo Mwanasheria Mkuu ataanzisha vitengo chini ya idara zinazoanzishwa chini ya kifungu cha 2 ya kifungu hiki au bila ya kuwepo idara atateuwa wakuu wa kitengo kwa masharti kama anavyoona inafaa kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa ofisi.

Hapa nilikuwa na suala labda Mhe. Spika, sikufahamu lakini labda niulize vipi bila ya kuwepo idara. Mhe. Spika, niende vile vile nambari 9 ujira wa utumishi wa ofisi ya kitaalamu na wasaidizi utafanywa kwa mujibu wa kinuni za utumishi wa umma, isipokuwa kwamba katika hali yoyote utaratibu wa kuajiri utafuatwa na ule utakaopatikana upatikanaji wa watumishi wazuri. Kwa kweli Mhe. Spika, sijafahamu namuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi anisaidie kifungu hiki kunifafanulia vizuri.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme kwamba nashukuru kwa niaba wananchi wangu wa Jimbo la Amani ninaunga mkono mswada huu.

Mhe. Spika: Mhe. Fatma tunakushukuru kwa kuokoa jahazi, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma aendeleze uokozi wa jahazi hili.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii adhimu kumshukuru subhana wataala kutujaalia kuwepo hapa leo tukiwa wazima wa afya na kuendelea na shughuli zetu ambazo zimetuleta hapa.

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia mswada huu ambao tumeletewa hapa mezani kwetu. Mhe. Spika, baada kutokea hayo yaliyotokea katika kipindi kidogo sana na umeona aliyeokoa jahazi ni mwanamke, kwa hivyo wanawake wanaweza. Mhe. Spika, hii inadhihirisha kwamba wanawake tukipewa nafasi zaidi ya hizi ambazo tunazipata hivi sasa basi tutaweza kufanya mambo mazuri zaidi. Nafikiri nimeeleweka vizuri. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwanza kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ambaye akishirikiana na watendaji kwa kuweza kutuletea mswada hapa Barazani. Mhe. Spika, mswada huu kama walivyotangulia kusema wenzangu ni mswada ambao ni muhimu sana kwa wakati wetu huu wa leo.

Nasema hivyo kwa sababu kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar ya 1984 kifungu cha 55 kimempa mamlaka Rais ya kumchagua Mwanasheria Mkuu. Ina maana kwamba kwa pamoja wetu tumeona umuhimu wa kuwepo Mwanasheria Mkuu, lakini hitilafu iliyokuwa imejitokeza kwamba Mwanasheria Mkuu huyu ambaye tumempa mamlaka makubwa kulikuwa hakuna sheria ya kumuongoza na kumuelekeza katika shughuli zake. Hilo lilikuwa ni kosa kubwa lakini tushukuru kwamba sasa hivi kosa hilo tunalirekebisha na *in shaa Allah* kwa kudra ya Mwenyezi Mungu tutaweza kufanikiwa na tutarahisisha shughuli zetu zote ambazo zinahusiana na sheria.
Mhe. Spika, mimi kwa kweli nisingependa kusema mengi kwa sababu sioni cha kusema kwa sababu naunga mkono takriban vifungu vyote vilivyokuwepo ndani ya mswada huu. Mhe. Spika, mimi kidogo nilikuwa nataka kuzungumzia katika kifungu ambacho kinasema kwamba atateuliwa Naibu Mwanasheria Mkuu akiwa na sifa ambazo zimetajwa hapa katika kifungu Nam.6.

Mhe. Spika, kwa muda huu tulionao kwa sasa hivi naona hizi *criteria* ambazo zimeekwa hapa ili ziwe ni sifa ambazo za kumchagua Naibu Mwanasheria Mkuu, mimi nahisi kwamba bado ni sifa ndogo hasa katika suala la elimu.

Mhe. Spika, sasa hivi Wazanzibari wengi sana wana elimu ya sheria hasa kwa digrii ya kwanza. Hapa tunataka kufanya ushindani na katika ushindani, unapotafuta mtu bora lazima uwe na *criteria* nzuri na bora zaidi ili katika wale watakaokuja kushindana basi wawe na sifa za juu sana. Kwa upande wangu nafikiria kwamba badala ya kuwa na digrii moja basi Naibu Mwanasheria Mkuu awe angalau ana digrii mbili zikihusiana na masuala ya sheria. Hayo ni mawazo yangu.

La pili, nilikuwa ninataka kumwambia Mwanasheria Mkuu tunao akinamama wengi ambao wana sifa hizi na hata kuwa na digrii ya pili. Sasa tutizame vile vile kipengele cha jinsia. Kama kunaonekana kama wapo akinamama

ambao wana uwezo kama huu ambao unatakiwa basi tusije tuka-*hasitate* kumpa nafasi ile, tusije tukasita kumpa nafasi kwa sababu yule ni mwanamke. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi hili ni ombi langu maalum na nafikiria litafikiriwa vizuri.

Mhe. Spika, vile vile nilikuwa nataka kuzungumzia suala la ambalo mwenzangu aliyetangulia amelizungumzia, suala la mikataba. Suala la mikataba tumeona mikataba mingi ambayo katika kipindi kirefu imekuwa ikisainikwa lakini ilikuwa na udhaifu wa kisheria.

Sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itakuwa na utaratibu maalum ambao utahakikisha mikataba yote itakayosainiwa itakuwa ni mikataba ambayo ni maslahi ya wananchi wa Zanzibar pamoja na maslahi ya taifa letu kwa ujumla. Mimi kwa hilo kwa kuwa aliyepewa ofisi hii ni mtu ninayemfahamu sana na ni makini na kwa kweli namuamini sana na nina hakika kwamba kwa upande huu basi ataweza kutekeleza wajibu wake vizuri, kwa sababu ni Mzanzibari ambaye kwa kweli anaipenda nchi yake.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mswada kwa asilimia mia na nawaomba wajumbe wenzangu waubariki mswada huu na vile vile tuombe Mungu Mswada huu utekelezeke kama tunavyotarajia.
Mhe. Spika, nakushukuru sana

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi kwenye mswada huu muhimu sana wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Lakini ya kutoa mchango naomba nikuarifu kwamba isionekane kuwa Wajumbe hawachangii kwamba tumekosa uwezo, lakini kwa kweli kutokana na bidii aliyoifanya Mwanasheria Mkuu ya kutupatia semina ambayo kila mjumbe aliyeshiriki katika semina ile alikuwa na ufahamu wa hali ya juu. Kwa hivyo kama si wajibu ule wa kuchangia tungesema kama inatosha kupiga kura na kusema uende moja kwa moja, kwa sababu alitupatia semina, akachambua neno kwa neno, kifungu kwa kifungu na kwa kweli mswada mmoja wa kukaa zaidi ya saa saba huoni uone kwamba wajumbe walifahamu sana juu ya mswada huu. Kwa hivyo Mhe. Spika, wale ambao hawatochangia basi ni kuwa wameufahamu siku ile na tusije tukaharibu yale mambo tuliyopewa.

Mhe. Spika, sasa baada ya utangulizi wangu huo naomba niende kwenye mswada na niipongeze serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuamua kuleta mswada huu ambao kwa kweli lengo lake ni kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kisheria.

Mhe. Spika, kama ambavyo tumeambiwa Mwanasheria Mkuu ametajwa kwenye Katiba ya mwaka 1984, lakini alikuwa yupo kwa mujibu wa agizo la Rais, alikuwa hayupo kwa mujibu wa kisheria. Kwa hivyo madhumuni makubwa ya mswada huu ni kuanzishwa ofisi hii kisheria ili iende sambamba na taratibu za nchi.

Kwa hivyo Mhe.Spika, pongezi za mwanzo kwamba ofisi hii kwamba kuwepo kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kisheria ili iende sambamba na Katiba yetu ya nchi ya mwaka 1984 na katika hilo mimi nichukue nafasi hii kuipongeza sana serikali kwa kuamua suala hilo.

Mhe. Spika, lakini Katiba inatambua kwamba Mwanasheria Mkuu ndiye msaidizi mkuu wa serikali kwa upande wa kisheria, na tumekuwa tukishuhudia kila inapokezea kesi mbali mbali hata kama kesi ataifanya mtendaji wa serikali mwengine lakini anayesimama Mahakamani ni Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo kuwepo kwa ofisi hii kisheria nadhani itasaidia hata utekelezaji wa majukumu yake mbele ya serikali kwenye utetezi wa serikali. Mhe. Spika, kifungu cha 4 kinaanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambapo itakuwa uhuru na yenye mamlaka ya kujiendesha ndani ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, nadhani hili ni jambo la busara kwamba ofisi hii tuiache iwe ofisi huru inayojitegemea katika utumishi wa umma ili kuweze kusaidia maendeleo ya nchi na katika sekta hii ya kisheria. Si vyema kabisa kuanzishwa ofisi hii kisheria halafu tukaingilia katika utendaji wake wa kazi, nadhani tukubali na serikali ikubali na wananchi wakubali kwamba ofisi hii tuiachie huru isiingiliwe katika mambo yake ya kisheria na tuwaache wafanye shughuli zao kwa mujibu wa sheria.

Lakini kifungu cha 5 (1) Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye mkuu wa ofisi. Mhe. Spika, Mwanasheria Mkuu atatekeleza kazi za jumla na maalum na kutumia uwezo wake aliyepewa na Katiba na sheria hii na sheria nyenginezo. Hili pia ni jambo muhimu kwa Mwanasheria Mkuu ndiye atakayekuwa mkuu wa afisi na atatekeleza majukumu yake kwa mujibu Katiba na Sheria hii.

Lakini vile vile tumeambiwa kwamba sasa kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu ambaye hapo zamani kulikuwa hakuna uhakika wa kupatikana kwake, ilikuwa ni utashi tu wa matakwa ya Rais aliyehusika kumchagua Naibu Mwanasheria Mkuu. Lakini sheria hii sasa hivi imehalalisha kifungu 6(1) kwamba Rais sasa atamteua Naibu Mwanasheria Mkuu ambaye ndiye atakayekuwa msaidizi mkuu wa Mwanasheria Mkuu.

Jukumu lake ni kwamba atawajibika kwenye maslahi, kufanya mikataba, wastaafu na utumishi mzima wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, nadhani ni jambo la busara vile vile Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa sababu yeye ndiye pekee anaingia kwenye Baraza la Wawakilishi, muda mwingi tunapokuwa kwenye Baraza la Wawakilishi anakuwa yupo hapa, kwa hivyo kuekewa Naibu Mwanasheria Mkuu kama ni mtendaji mkuu wa afisi hii nadhani ni jambo la busara. Kwa hivyo naomba Wajumbe wenzangu tuunge mkono kwamba kifungu hiki kipite ili Naibu Mwanasheria Mkuu aweze kupata nafasi ya kutosha kumsaidia Mwanasheria Mkuu hasa pale anapokuwa nje ya afisi. Tunatambua kwamba muda mwingi Mwanasheria Mkuu anakuwa yupo ndani ya Baraza kama ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini kuwepo Naibu Mwanasheria Mkuu kutasaidia afisi hii kuwa na mtendaji madhubutu hasa kwa upande wa maslahi, mikataba na masuala mazima ya utumishi wa umma.

Mhe. Spika, jambo jengine muhimu ni kwamba Mswada huu sasa umeweka masharti kwamba mikataba yote ambayo itaingiwa na serikali kwa maslahi ya taifa, lazima ipate baraka ya Mwanasheria Mkuu, ni jambo zuri. Tumeshuhudia mara zote kwamba nchi hii inapata hasara kwa mikataba isiyozingatia vigenzo. Nchi hii inaingia hasa kwa watendaji wasiotambua umuhimu wa kuwa na mikataba inatambua sheria. Kwa hivyo kifungu hiki ambacho kimeamua sasa kwamba mikataba yote ya nchi na mimi niseme yote; iwe ya serikali kuu, mashirika na taasisi zake basi lazima ipate baraka ya Mwanasheria Mkuu ili yeye ndiye dhamana wa mambo yote ya kisheria.

Kwa sababu ikitokezea kushtakiwa serikali, yeye ndiye anayesimama mbele ya Mahakama kwa ajili ya kutetea hoja ya serikali. Kwa hivyo naunga mkono kabisa kwamba mikataba ya serikali kwa ngazi zote basi ni vyema isimamiwe na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa sababu yeye ndiye mdhamini mkuu wa serikali kisheria.

Mhe. Spika, jambo jengine ni masuala ya fedha. Kifungu hiki kimeeleza vile vile kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu ndiye atakayekuwa mdhamini kama *accounting officer* wa afisi hii. Hapo awali ilikuwa kuna mtizamo tofauti lakini kutokana na majukumu ya Mwanasheria Mkuu kulikuwa na wengine walikuwa na mawazo kwamba Mwanasheria Mkuu abakie kuwa ni *accounting officer* na kuna wengine walikuwa na mawazo kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu ndiye awe *accounting officer*. Mimi kwa upande wangu naona pamoja na majukumu mengi aliyekuwa nayo Naibu Mwanasheria Mkuu lakini tumbakishe kuwa ni *accounting officer* kwa upande wa afisi yake.

Mhe. Spika, jambo jengine ningelisema kwa pongezi kubwa Mwanasheria Mkuu afisi yake amekubali tangu kwenye semina kwamba suala la kuwadhibiti, kuwasimamia wanasheria wa Baraza la Wawakilishi, wanasheria wa Afisi ya Mahakama na wanasheria wa Afisi ya Muendesha Mashtaka libakie katika afisi zao husika.

Mimi nichukue nafasi hii kabisa kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwamba uamuzi wake wa kuwabakisha wanasheria wa Baraza kuwa ni wanasheria wa Bara ni wa msingi. Kwa sababu huu ni muhimili wa dola kama mihimili mengine. Kwa hivyo nichukue nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwamba amekubali wazo la Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi afisi wanasheria wake wajitegemee sambamba na wale wanasheria wa Mahakama na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Katika hilo Mhe. Spika, nilitaka kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu kwamba ameona umuhimu wa kuibakisha Baraza la Wawakilishi kwa sababu ni muhimili wa dola na kwa kasi ile ile nadhani itakuwa rahisi sasa kutusaidia kurekebisha ile sheria ya utumishi wa umma, ili mambo yote yanayohusi Baraza la Baraza la Wawakilishi yabakie kwenye msimamo wa Baraza la Wawakilishi kama ni muhimili wa dola.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ningelichangia haraka haraka ni suala zima la Mwanasheria Mkuu kuwa ni kiongozi wa Mawakili. Mhe. Spika, pia hili ni jambo zuri kwamba Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa sheria hii atakuwa ndiye kiongozi wa Mawakili, na ikitokezea kuhudhuria Mahakamani, Mwanasheria Mkuu ndiye

atakayepewa nafasi ya mwanzo kuhudhuria katika kikao cha Mahakama. Hili ni jambo zuri kwa sababu yeye ndiye Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini ndiye kiongozi wa mawakili. Kwa hivyo nadhani na hili lipongeze kwamba limekaa vizuri katika upande huu wa kisheria kwamba yeye mtu wa mwanzo wa kupewa nafasi ya kuingia Mahakamani iwapo kutakuwa na mawakili wengine kama ni kiongozi wa mawakili wote.

Mhe. Spika, nadhani kama nilivyosema mwanzo mswada huu Mwanasheria Mkuu aliumaliza siku ya mafunzo ya semina, alitoa ufafanuzi neno kwa neno na kwa kweli alikuwa makini sana na bahati nzuri nilialikwa niliona kwamba niseme hayo kwa ajili ya kutoa baraka zangu, lakini kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani niunge mkono mswada huu asilimia mia kwa mia. Niwaombe wenzangu kama si makosa ya uandishi basi tuupitishe asilimia mia kwa mia.
Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu Mtukufu Azza Wajaallah, kwa kutuamsha leo siku ya Ijumaa tukiwa hai na wazima wa afya na leo tukiwa tunaujadili mswada unaohusu ofisi adhimu, ambao kwa sasa pia inaongozwa na mtu adhimu sana, Mhe. Othman Masoud Othman.
Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa ya kusema machache kuhusiana na mswada huu. Tatu, Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa hatua yake na Wizara anayoiongoza, kuweka historia leo kwa mara ya kwanza Zanzibar kuleta mswada unaoanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, bila shaka yoyote kwa nchi kongwe ambayo ina ustaarabu wa muda mrefu kama ilivyo Zanzibar katika Bara la Afrika, sio ajabu kama ni katika nchi za mwanzo kabisa ambazo zilijenga misingi mizuri sana ya mifumo ya kisheria na kuanzisha taasisi mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Lakini kama walivyoeleza wenyewe kwa muda mrefu ofisi hii haikuwa na sheria mahsusi hasa ambayo ilikuwa inasimamia na kuongoza shughuli zake. Sasa leo Mhe. Abubakar Khamis Bakary akiwa ni Waziri wa Katiba na Sheria, kuchukua hatua ya kuwasilisha mswada kwa ajili ya kuanzishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kuweka utekelezaji wa majukumu na uwezo, pamoja na mambo yanayohusiana na hayo ni kitendo cha kihistoria. Mimi naomba nimpongeze sana kwa kuingia katika historia leo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kumalizia pongezi na shukrani Mhe. Spika, naomba vile vile nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa sababu naamini na yeye ametoa mchango mkubwa sana uliopelekea mswada huu leo kufika mbele ya Baraza lako tukufu. Umahiri na uwezo wake unaonekana Mhe. Spika, kwa sababu hiki chakula kajipikia mwenyewe. Mhe. Spika, hakuniambia, lakini naamini kabisa kama kutakuwa na mswada ambao utakuwa ameshiriki sana katika kuusimamia na kuuandaa basi utakuwa ni huu. Matokeo yake ndio maana leo kila ukitamka hapo majadiliano yanaendelea, meza huku zinakutazama sana, kwa sababu mpishi alikuwa kakamilika hakubakisha katika viungo, mpaka hata sisi huku wengine tuliozowea kutumwa tumwa kupeleka vitu vichache jikoni, leo tumekwama kabisa Mhe. Spika.

Sasa baada ya maelezo hayo ya utangulizi Mhe. Spika, naomba niseme machache. La kwanza kabisa ambalo nataka kulizungumza ni hili la kihistoria. Nilisema katika maelezo yangu ya awali kwamba nchi yetu ni katika nchi zenye ustaarabu mkongwe kabisa katika Bara la Afrika. Mhe. Spika, moja ya sifa na vigezo vya watu wastaarabu ni uwezo wao wa kujiundia kanuni na sheria zinazoongoza mambo yao, maana jamii ambazo hazikuendelea na hazikustaarabika Mhe. Spika, huishia kutumia maguvu na vurugu katika kumaliza mambo yao. Lakini watu wastaarabu utawajua kwa sababu tangu mwanzo huwa wanaweka kanuni katika kuongoza mambo yao. Zanzibar Mhe. Spika, tuliopitia katika historia ya *organization* ya jamii zetu, tunajua kwamba katika taratibu za utawala tangu karne na karne, tangu zama za Madiwani wa Pemba, Masheha wa Tumbatu, Mwinyi Wakuu katika kisiwa cha Unguja, kote kulikuwa kuna taratibu zilizoanzishwa na zilizotangulia kabla ya hapo, ambazo zilikuwa zimeweka nidhamu nzuri za uendeshaji wa mambo. Hiyo Mhe. Spika, inaonesha tu jinsi nchi yetu ilivyokuwa ina historia refu sana katika masuala mazima ya kuendesha mambo yake.

Mhe. Spika, sio tu katika kuanzisha taratibu za utawala, lakini na kuanzisha kanuni zinazoongoza taratibu za utawala, masuala ya utatuzi wa migogoro yalikuwa yamewekwa wazi wazi katika nidhamu zote za utawala waliokuwa wakitawala kuanzia Masheha wa Tumbatu, Madiwani kwa Pemba na Mwinyi Wakuu kwa upande wa Unguja. Yote hayo ukiangalia katika historia yako wazi wazi.

Lakini ninalotaka kuligusia ni lipi Mhe. Spika. Unaweza ukawa na nidhamu za utawala wa ndani Mhe. Spika, lakini kilele cha kuonekana kwamba wewe umevuka kiwango cha ustaarabu ni mahusiano yako baina ya nchi yako na nchi nyengine.

Mhe. Spika, leo nimekuja na moja katika vitabu vilivyoandikwa mapema sana kuhusu historia ya Zanzibar na watu wake. Hiki ni kitabu kilichoandikwa na *Ingrams* mwaka 1930, kinaitwa *Zanzibar it's history it's People.* Humu kumechambuliwa mambo mengi Mhe. Spika, lakini katika ukurasa wa 267 mpaka 273 inaelezea Zanzibar na jinsi ilivyokuwa na historia katika masuala ya sheria, kinahusu hasa *law* kimeandikwa.

Katika ukurasa wa 268 Mhe. Spika, mpaka 272 mwandishi *Ingrams* ambaye alikuwa ni mtumishi katika Serikali ya Kikoloni au Utawala wa Kiingereza uliokuwepo Zanzibar hapa. Anaelezea *International Law* katika Zanzibar. Naomba ninukuu sehemu ndogo tu Mhe. Spika, katika ukurasa wa 268;

> "*It may seem curious to consider that there are any traces of International Law among the natives of Zanzibar, though of course Zanzibar is a well defined position as an independent state and treaties with it many of which are still in force were entered into by many foreign powers. But the study of the history of the natives shows that they have a well defined idea of the nature of an international obligation".* Mwisho wa kunukuu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikiifasiri kwa haraka haraka tu inasema kwamba mtu anaweza kuwa na shauku ya kujiuliza kwamba je, kuna angalau dalili za kuwepo sheria ya kimataifa miongoni mwa wenyeji wa Zanzibar. Pamoja na kutambua kwamba Zanzibar ina hadhi inayotambulikana kama ni nchi huru na ambayo imefika kuingia mikataba na madola makubwa na mikataba hiyo mpaka leo wakati anaandika kitabu hiki mwaka 1930 anasema ina nguvu. Lakini anasema utafiti umeonesha katika historia ya wenyeji kwamba wanao utaratibu unaotambulika wa kufahamu nidhamu ya wajibu wao katika sheria za kimataifa.

Hivi ndivyo Zanzibar inavyozungumzwa katika historia Mhe. Spika. Mwaka 1930 anaandika haya, lakini haya hayazungumzii Zanzibar 1930 Mhe. Spika. Anazungumzia utafiti wake wa *native* anaita yeye, wenyeji wa Zanzibar karne na karne kabla ya kuwepo kwamba tayari walikuwa na *concept* na *nature of obligation* katika *international law*. Mhe. Spika, hiyo ndiyo Zanzibar, wasiyoijua waitambue.

Kwa hivyo, ninachosema kwa nchi yenye historia kama hii Mhe. Spika, ni jambo la faraja kwamba leo tunaivisha taji historia hii. Tunaivisha taji kwa kuunda sheria sasa kwa mfumo ambao ulikuwepo katika mahakama, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwamba sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inaanzishiwa sheria yake rasmi ambayo ikisaidiana na vifungu vya Katiba ya Zanzibar vilivyotajwa hapa, sasa itakuwa ndio inaongoza shughuli za ofisi hii.

Mhe. Spika, wakati Zanzibar inafanya hayo katika historia kulikuwa na jamii nyengine hata ule ustaarabu wa kuwa na mavazi ya binadamu ulikuwa bado haujaanzishwa, Zanzibar ilikuwa imefika huku. Sasa Mhe. Spika, niende katika mswada wenyewe.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa jumla sidhani kama atatokea Mjumbe kwamba atakuwa na nyongeza sana katika vifungu kuliko yale ambayo yameshaingizwa humu na yamepitia katika semina ile na katika kazi za Kamati. Lakini yako mambo machache ambayo ilikuwa naomba kuyatilia nguvu.

Kwanza Mhe. Spika, ni kifungu cha 8 cha mswada ndio ambacho nilikuwa nataka nikizungumzie, kifungu hiki kinazungumzia muundo wa ofisi.

Kifungu cha 8(1) kinasema;

> "Mwanasheria Mkuu atakuwa na dhamana ya utendaji wenye ufanisi na unaofaa wa ofisi na anaweza kwa madhumuni hayo na kwa kushauriana na mamlaka husika ya utumishi wa umma, kuunda muundo wa ofisi katika vitengo kama atakavyoona inafaa, au anaweza kupendekeza kuundwa idara ndani ya ofisi kama atakavyoona inafaa".

Sasa Mhe. Spika, jana kidogo nilikuwa nikimuulizauliza Mhe. Mwanasheria Mkuu mawazo yake kuhusiana na hili, kwamba je hatuoni haja ya kutaja baadhi ya hizi idara au vitengo ndani ya mswada huu. Akanipa maelezo yaliyonikinaisha Mhe. Spika, kwamba ili kuwa na unyumbufu ni vizuri kuiacha hivi na mimi kimsingi naikubali Mhe. Spika. Lakini wakati nakikubali kifungu kama kilivyo nilikuwa naomba katika huko kufikiria mamlaka

ambayo sheria hii itakuwa inampa, namuombea kwa muda mrefu Mwanasheria Mkuu aliyopo aendelee kushika nafasi hii, basi nilikuwa naomba afikirie Mhe. Spika, vitengo viwili.

Kitengo cha kwanza ni hiki ambacho kimeshazungumzwa sana na Wajumbe hapa, katika mawazo yao kwenye kupongeza wamepongeza sana Mhe. Spika, na mimi nitakuja baadae kidogo huko, juu ya suala la mswada huu wa sheria sasa kuweka utaratibu kuhusiana na masuala yote yanayohusu uandaaji na ufungaji wa mikataba ambayo inahusisha serikali na taasisi zake.

Sasa Mhe. Spika, nilikuwa nadhani katika vitengo vya mapema sana ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu akifikirie basi ni kuwa na kitengo mahsusi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambacho kitakuwa kinasimamia mikataba katika serikali. Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu gani, kwa sababu tumeona hapa katika shughuli za Baraza hili tangu limeanza mwaka 2010, mijadala mbali mbali, Kamati teule mbali mbali zilizoundwa kwamba kuna matatizo makubwa sana katika masuala yanayohusu uandaaji na utekelezaji wa masharti ya mikataba mbali mbali ambayo inahusisha serikali na taasisi zake kwa upande mmoja na taasisi nyengine hasa taasisi binafsi Mhe. Spika. Tumeona Mhe. Spika, kwamba kuna matatizo makubwa sana katika taasisi za serikali, kuanzia Wizara zenyewe, idara zake, mashirika, kamisheni kufuata masharti ya sheria ya manunuzi ya umma kwa mfano, limejitokeza sana Mhe. Spika hili mara kwa mara.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Spika, kama kuna sehemu ambayo inataka kuongezewa nguvu katika utendaji wa serikali basi ni muongozo kutoka ofisi hii ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, katika masuala yanayohusu uandaaji wa mikataba na utekelezaji wa masharti yake. Najua haitokuwa kwa kila kitu Mhe. Spika, kuna mambo mengine kwa taratibu za serikali lazima Wizara zenyewe na ofisi zake zitakuwa zinasimamia na tunategemea wale wanaoongoza maana yake wafanye vizuri.

Lakini Mhe. Spika, nilichokuwa nakizungumzia ni kwa ile mikubwa, kwa sababu hata mswada huu unazungumza hivyo, kwamba mikataba mahsusi ambayo imefikia kiwango fulani au hadhi au sifa ambayo inapaswa isimamiwe huku na Ofisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa nilikuwa nasema, lakini kwa jumla katika kusaidia serikali na pengine tushajihishe utaratibu huo kwamba ofisi zetu mbali mbali kuanzia wizara, maidara, mashirika, kamisheni zinapoona jambo kama hilo basi zitake ushauri katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Sasa nilikuwa nasema katika hicho kifungu cha 8(1) anapoona vitengo, tutizame sana haja ya kuwa na kitengo mahsusi cha mikataba na kukipa nguvu ili kiweze kuisaidia serikali kwa jumla yake, ili haya mambo ambayo yanaipatia sifa mbaya Zanzibar, ya kutajwa katika masuala mbali mbali ya ufisadi, watendaji na wakuu wa serikali kujitajirisha na kujinufaisha binafsi kama ilivyoonekana katika Kamati mbali mbali ndani ya ripoti zake hapa yaweze kupungua. Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alifikirie.

La pili katika hilo hilo la muundo, nilikuwa namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu azingatie huko tunakokwenda Mhe. Spika, hapana shaka yoyote na kila siku zikienda ukisoma tafiti mbali mbali na taarifa zinazochapishwa katika mitandao huko, inajulikana kwamba Zanzibar Mhe. Spika, ina utajiri mkubwa wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia. Nchi nyingi Mhe. Spika, pamoja na kuvumbua au kugundua kuwepo kwa gesi asilia za mafuta, lakini hazikusaidia sana rasilimali hizi maisha ya wananchi wake kwa sababu kulikuwa kuna wakubwa fulani katika nchi walijinufaisha wao.

Mfano mzuri Mhe. Spika, sasa hivi ukifuatilia yanayotokea *Equatorial Guinea*, ni mfano mzuri sana Mhe. Spika, kwamba ni wakubwa wa serikali na wa nchi wamejifanya ndio utajiri wao. Nilikuwa Uingereza hivi karibuni Mhe. Spika, na mmoja katika *members* wa *House of Lords* Uingereza, nilikutana naye kule akaniambia kwamba Afrika haitabadilika mpaka pale viongozi wake watakapojitofautisha, kwamba wao *they are not the owners of the wealth of African Nations but they are the custodians of the wealth of African Nations.* Kwamba viongozi wa Kiafrika wabadilike wasijione wao ndio wamiliki wa utajiri wa nchi zao, lakini wajione wao kwamba ni watunzaji na wasimamizi wa utajiri wa nchi zao.

Sasa Mhe. Spika, nasema ukitizama uzoefu umeonekana nchi nyingi hazijafaidika kama hatukujiandaa mapema kusimamia suala hili. Mimi najua kwamba Baraza hili lilishafanya maamuzi mwaka 2009. Jana nilisema na kwa hili Mhe. Spika sitochoka kusema mimi kwa suala hili la mafuta na gesi, mpaka niwe nimelifikisha mwisho katika Baraza hili, pamoja na wenzangu ambao naamini na wewe mwenyewe Mhe. Spika, naamini kama ulivyokuwa mwaka 2009 tutasimamia kwa pamoja kuona kwamba hili linafikishwa mwisho.

Mhe. Spika, nilitaka kusema kwamba tunahitaji tujipange vizuri, vipi utatumika utajiri huu na moja katika maeneo makubwa sana ni vipi tunajiandaa katika kuwa na uwezo wa kujadiliana masuala yote yanayohusu usimamizi na uendeshaji wa sekta hii ya mafuta na gesi asilia.

Mhe. Spika, sera ya nishati ya Zanzibar ya mwaka 2009 imeweka wazi kwamba chombo hiki unachokiongoza wewe Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi kina jukumu la kupitia na kuidhinisha mikataba yote itakayokuja kuhusu sekta ya mafuta na gesi asilia, ni lazima iidhinishwe na Wawakilishi wa wananchi katika chombo hiki unachokiongoza Mhe. Spika. Sasa kwa sababu hiyo Mhe. Spika, hatua ya kuja kuidhinishwa ni ya mwisho, lakini hatua ya majadiliano, hatua ya kujiandaa na hatimaye kufungwa mikataba ile itasimamiwa na serikali na bila shaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itakuwa na nafasi kubwa sana.

Kwa hivyo, nilichokuwa nakiomba tena katika kifungu cha 8(1) Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu azingatie vile vile kwamba huko tunakokwenda uchumi wa Zanzibar sehemu kubwa badala ya kuwa karafuu na utalii, itakuwa ni uchumi wa mafuta na gesi asilia, na kama ni hivyo basi ni lazima kwa mawazo yangu mimi Mhe. Spika, tuwe na kitengo maalum katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambacho kimejikita na hilo tu moja, ili utajiri huu uliomo katika bahari ya Zanzibar, uliokuwa pengine karibu na visiwa vya Zanzibar uje uwanufaishe watu wa Zanzibar wenyewe na usije ukaishia katika mifuko ya watu wachache. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo pia katika sehemu ya muundo alizingatie Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, nikondoka hapo naomba sasa nije katika vifungu ambavyo, kusema kweli nataka kupongeza. Nimefurahi sana katika maudhui ya mswada huu, katika kifungu cha 14, 16 na 22 Mhe. Spika, kwamba kunazungumzwa masuala yanayohusu nafasi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika uandaaji au upitiaji wa mikataba ambayo inahusu serikali. Mhe. Spika, kifungu cha 14(h) kiko katika ukurasa wa 323 wa gazeti rasmi la serikali, kinahusu kazi za ofisi, kinasema;

Kifungu cha 14(h)

> "Kutoa ushauri wa kisheria kwa serikali na taasisi za umma katika kupatana na kutayarisha mikataba ya kibiashara na mikataba mengineyo isiyokuwa ya kibiashara kwa niaba ya serikali". Hicho ni 14(1) (h).

Lakini kifungu cha 14(1) (l) vile vile kinasema;

> "Kushiriki katika hatua zote za awali za matayarisho ya mikataba, utimizaji na utekelezaji wa mikataba yote yenye sifa maalum ambayo serikali ni sehemu ya mikataba hiyo".

Hivyo ni vifungu viwili Mhe. Spika, katika kifungu cha 14 kazi za ofisi inahusu mikataba. Lakini katika kifungu cha 16 vile vile, uwezo wa Mwanasheria Mkuu na ofisi.

Kifungu cha 16(h) kinasema;

> "Kutunza madaftari ya kesi na mikataba yenye sifa inayostahili ambayo serikali ni sehemu ya mikataba hiyo".

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, kifungu cha 22, hiki sasa ndio kinazungumzia hasa uandaaji hati za kisheria za serikali na katika kifungu cha 22 hiki kinazungumzia pamoja na mambo mengine mikataba ambayo itakuwa inaijumuisha serikali kwa kipindi kirefu sina haja ya kukinukuu.

Sasa Mhe. Spika, awali nilipoupata mswada huu ulikuwa unanitia mashaka kwa sababu ukiondoa lile jukumu lake la kushiriki katika kuandaa na kutoa ushauri, kidogo nilikuwa napata matatizo ambapo nashukuru wenzangu waliopata nafasi ya kushiriki semina walikiona, na wakatoa rai ambayo nashukuru kwa usikivu wake Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu wamekikubali, kwamba sasa tunaongeza kifungu cha 22(2), katika haya marekebisho ya mswada wa sheria uliosainiwa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria katika ukurasa wa 4.

Mhe. Spika, naomba tufanye marekebisho kidogo, yale maelezo ya pembeni yameandikwa kifungu cha 24, wakati usahihi inapaswa kiwe ni kifungu cha 22, imesema kuongeza kijifungu cha (2) mara baada ya kijifungu cha (1) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo. Hii inaongezwa kule kwenye kifungu cha 22 sasa, kwamba miongozo na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu chini ya aya (c), (d), (f) na (g) yataziwajibikia ofisi na taasisi za umma. Afisa yeyote wa umma anayehusika na mkataba ambaye atatekeleza jambo lolote kuhusiana na mkataba husika, kinyume

na miongozo iliyotajwa katika kifungu hiki, atachukuliwa kuwa amefanya uzembe na atawajibika kwa lalamiko lolote na hasara inayoweza kutokea. Hili nalipongeza sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kama lingekuwa halikuingizwa hili, lakini najua kisheria mara nyengine vitu sio lazima vitaje wazi wazi namna hii. Lakini unapokuwa na watendaji mara nyengine wababaishaji Mhe. Spika, na tunawaona mara nyingi wanavyowahangaisha mawaziri wetu humu, katika mambo mbali mbali kuwashauri, wanaweza wakatumia mwanya uliokuwemo mle wakafanya wanavyotaka. Lakini hili la kupelekea kwamba sasa tuna kifungu tumekiongeza kijifungu kidogo cha (2) katika kifungu cha 22, ambacho kinaweka sharti hili la kuwafunga kutekeleza muongozo ambao unatolewa katika Ofisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, hili Mhe. Spika, ni la kupongezwa sana. Ni imani yangu kwamba katika kile kitengo cha mikataba basi suala hili litazingatiwa ipasavyo.

Vile vile Mhe. Spika, kifungu cha 20 kinahusu maoni ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa msimamo wa serikali. Mhe. Spika, kifungu hiki kinasema;
Kifungu cha 20(1)

> "Ushauri wa kisheria wa Mwanasheria Mkuu uliotolewa chini ya masharti ya sheria hii, utabaki kuwa msimamo wa kisheria wa serikali juu ya jambo hilo, isipokuwa kama Rais ataelekeza vyenginevyo, au umefanyiwa mapitio vyenginevyo na mahakama yenye mamlaka".

Mhe. Spika, kifungu hiki kimetoa mamlaka yaliyopaswa yawepo hasa, kwamba anayeweza kutengua ni ama Rais ambaye ndiye mwenye ridhaa ya watu katika kuongoza nchi hii au mahakama kwa mujibu wa Katiba yetu ina mamlaka mbali na aliyopewa ndani ya katiba, lakini pia ina mamlaka au uwezo wa kimaumbile kabisa wa kuweza kupitia chochote na kutoa maelekezo mengine.

Hili Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba kuingizwa kwa kifungu hiki sasa ule upungufu uliokuwa ukijitokeza kwa baadhi ya wakati, kwamba Ofisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu inatoa maelekezo au msimamo fulani, lakini halafu wengine wakachukulia kuwa ni jambo la kawaida tu na hawalifuati kikamilifu utakuwa umeondoka. Hili Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba haitakuwa kwa mambo yanayohusu ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tu, lakini hata kwa mfano katika majadiliano yanayohusu masuala ya Muungano, msimamo utakaokuwa unatolewa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa niaba ya ofisi, utachukuliwa kuwa ndio msimamo rasmi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wengine wote Mhe. Spika, kwa maana hiyo wakiwemo mawaziri, watawajibika kuheshimu msimamo ambao umetolewa pale, isipokuwa kama utakuwa umeteuliwa na Rais mwenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili pia limenifurahisha sana.

Mhe. Spika, nimalizie kidogo katika kifungu cha 29. Pamoja na kuusifu mswada huu, mwanzoni kidogo nilipata mashaka na kifungu hiki. Kifungu hiki cha 29 kinazungumzia mashirikiano na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Spika, nilipata matatizo kwa sababu nilikuwa najiuliza hizi ni ofisi mbili ambazo kila moja inajitegemea na Katiba imetoa uhakikisho wa mamlaka yake na uhuru na uwezo wake. Huko tulikotoka shughuli zile za DPP kwa kiasi fulani pia zilikuwazinafanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, sio zote lakini zilikuwa nyengine zikifanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Lakini ilipokuja kuanzishwa ofisi hii ambayo Mhe. Spika, nashkuru na nafurahi kwamba nilikuwa sehemu ya historia mwaka 2002 kwamba ilikuwa ni matokeo ya muafaka wa pili uliosainiwa mwaka 2001. Tuliokuwa katika kamati zile za mashauriano baina ya vyama vyetu viwili vya CCM na CUF. Lakini baadae katika tume ya Rais ya pamoja ya usimamizi JPAC ambayo tumo si haba humu ndani ambao tulipata nafasi ya kutumikia mule, ilipelekea kuishauri serikali kusimamia mabadiliko ya Katiba au marekebisho ya katiba ambayo ndio yalianzisha Ofisi ya DPP. Sasa ndio nikawa na wasi wasi kwamba je, tunataka kutafuta mlango mwengine tena wa kumbanabana. Lakini baada ya kukisoma vizuri niliridhika kwamba kinachozungumzwa hapa ni mashauriano ya kikazi ambayo ni ya kawaida.

Mhe. Spika, nataka nitumie nafasi hii kutoa tahadhari kwamba tubakishe kuwa lengo la kifungu hiki ni mashauriano au mashirikiano, lakini isije ikatafsirika kwa vyovyote kwamba ni kuingiliana katika kazi zao. Nikisema hivi Mhe. Spika, sina wasi wasi na mtu aliyepo hivi sasa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, uadilifu wake, umahiri wake na umakini wake. Bahati nzuri yeye mwenyewe kabla ya kuwa Mwanasheria Mkuu alikuwa ni DPP na ameacha historia kubwa na nzuri kabisa, kama kawaida yake Mhe. Spika, kila anapoingia huyu ana sifa ya kuacha rikodi nzuri kama hizo.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu ni kwamba unaweza ukawa na mtu muadilifu leo, lakini hii ni ofisi sio mtu. Unaweza ukawa na mtu mwengine kesho akataka kutumia vibaya dhana ambayo imewekwa katika kifungu hiki. Lakini

nasema kimaandishi imekaa vizuri kabisa na kama utakuwa una wasimamizi wazuri wa sheria katika mahakama, katika serikali na kwa Rais mwenyewe, au hata huyo DPP mwenyewe hatokubali kwa sababu kifungu hiki hakitoi mwanya huo. Kwa hivyo, ilikuwa nataka kutahadharisha tu kifungu hiki kisije kikatumika, kwa sababu hivi tunavyozungumza Mhe. Spika, tunasoma katika magazeti huko, kuna malumbano baina ya Polisi na Ofisi ya DPP.

Mhe. Spika, Katiba imetoa mamlaka wazi wazi kwa Ofisi ya DPP kusimamia masuala ya uchunguzi wa mashtaka na kusimamia kesi, lakini kuna mvutano huko na unajiuliza kwamba ni kiasi gani taasisi nyengine za serikali zinaheshimu mamlaka ya DPP ambayo yako kikatiba na uwezo wake unalindwa kikatiba Mhe. Spika. Kwa hivyo, nilikuwa nasema mambo kama haya yanaweza yakatokezea, ni imani yangu kwamba mwanya au utaratibu huu wa mashirikiano uliotolewa katika kifungu cha 29 hautakuja kutumika vibaya na watu wengine watakuja katika ofisi siku za mbele huko kuja kuingilia uwezo wa DPP.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, katika taratibu za uandishi tu yale marekebisho ambayo yamefanywa ambayo yaliliingiza Baraza la Wawakilishi. Hili nalisema kwa jumla tu Mhe. Spika, naamini Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu watanikubalia pendekezo langu dogo tu. Kwamba nadhani katika uandishi, labda ili nieleweke na nitoe mfano mmoja tu.

Mhe.Spika, naona imeandikwa Baraza la Wawakilishi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama. Labda nitoe mfano katika huu waraka wa marekebisho alioleta Mhe. Waziri ukurasa wa mwanzo pale, kifungu cha 3 chini, unaonekana mfano kama huo. Nilichokuwa nataka kusema Mhe. Spika, nadhani katika uandishi, Mahakama ni muhimili wa dola wa aina yake na hadhi yake. Kwa hivyo, nadhani kiuandishi ulipaswa ufuatane na Baraza la Wawakilishi na usitanguliwe na ofisi ya DPP. Kwa hivyo, hii ni katika masuala ya uandishi Mhe. Spika, nasema kwamba ni vizuri ikawa ule mteremko unaonekana vizuri zaidi, kwamba Baraza la Wawakilishi, Mahakama na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Ni chombo cha kikatiba lakini sio muhimili wa dola kama ilivyo Mahakama na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nilianza kwa kutoa pongezi na shukrani. Nataka tena nirudie hilo kwamba nawapongeza sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa hatua ya kuleta mswada huu, leo tunaandika historia nyengine Zanzibar, katika masuala yote yanayohusu utendaji wetu wa masuala ya sheria. Ni imani yangu kwamba kitendo cha leo au kesho sijui, kwa muongozo wako Mhe. Spika Baraza hili kuupitisha mswada huu, tutakuwa tumejiwekea kinga nyengine na ngao imara ya Zanzibar katika kusimamia maslahi yake. Zaidi nitumie fursa hii kumpa nguvu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na kumpa moyo kwamba aendelee na asiyumbe kuwa mtetezi imara wa haki na asiyumbishwe na kingine chochote.

Mhe. Spika, katika eneo moja ambalo mimi namuheshimu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu, ni suala la kusimamia haki za Zanzibar linapokuja suala la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Waraka wake ambao alitutolea katika semina ambapo wananchi wa Zanzibar wote walipata nafasi ya kuusikia, kwa kupitia matangazo ya moja kwa moja, ulipongezwa na wengi wanaoipenda nchi hii Mhe. Spika. Maoni yake aliyoyapeleka katika Tume ya Mabadiliko ya Katiba, waliopata fursa ya kuyaona wameyasifu na kuyapongeza mengi. Mimi kama ningekuwa nataka kuishauri serikali katika hili la kuwa na msimamo wake basi nadhani ningeishawishi sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwamba yale maoni yaliyotolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa nafasi yake binafsi nadhani basi yangechukuliwa na yakawa ndio msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika mchakato mzima huu wa Katiba. Kwa sababu kama alivyo yeye mwenyewe yanawakilisha umakini, yanawakilisha uadilifu, yanawakilisha haki na haki inatiririka katika waraka ule Mhe. Spika, kama inavyotiririka ninavyoamini katika damu yake Mhe. Othman Masoud Othman.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wote wauunge mkono mswada huu, kama kungekuwa na asilimia zaidi ya 100 basi ningesema kwa zaidi ya asilimia 100. Lakini kwa sababu kiasilimia ni asilimia 100, basi naomba tuunge mkono kikamilifu na tuwape nguvu na tuwape moyo waweze kutekeleza kazi zao. Mhe. Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu tunakushukuru. Muda umefika sasa niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea katika orodha yangu ninalo jina la Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia jambo nilikuwa na jambo moja dogo na zito kwa kiasi, ambalo kwa upande wangu niliona kwamba niweze kulizungumza hili, ili tuweze kuangalia namna gani ya kuweza kuliingiza humu.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 14(1) sehemu ya tatu kuhusu kazi za ofisi kuna kazi ambazo zimeainishwa hapa kutoka (a) mpaka (p) nimeziona. Lakini kuna kifungu kimoja ambacho kama kawaida yetu tunapofika hapa na tunapozungumzia maendeleo katika nchi, basi mara nyingi sana nchi inapopata maendeleo na mbinu za ghilba pia nazo huwa zinapatikanwa.

Sasa katika hili Mhe. Spika, ni kwamba nimejaribu kuangalia kwa undani kabisa kazi zitakuwa zinafanywa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Lakini sikubahatika kuona kifungu chochote ambacho kitakuwa kinatoa adhabu kwa wale ambao watakuwa wanafanya makosa.

Kwa mfano, wale mawakili watakaokuwa si wa serikali, lakini watakuwa wanavaa majoho ya serikali kwa ajili ya kwenda kufanya kazi na katika dunia yetu ya utandawazi huu mambo kama haya kwa sasa yanawezekana.
Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa labda atuelezee kwa nini ikiwa kipengele hichi hakuna au akiona kina umuhimu kwa umuhimu wake, basi akichukue nacho ili kiwemo kwenye mswada huu ambao tunataka kuupitisha hapa na wala isije ikawa baada ya kipindi fulani tunarejea tena kuujadili mswada huu kwa ajili ya kuona kwamba kuna mapungufu ya namna kama hii.

Vile vile ukiangalia na mengine kwenye mswada huu kwa kweli kazi ambayo imekwisha kufanywa Mhe. Spika ni kubwa tena ni nzuri.

Kwa maana hiyo, mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi walionichagua kunifikisha hapa tunaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Lakini hicho kipengele ambacho nimekiona humu naomba kiangaliwe kwa umuhimu wake na ikiwa upo uwezekano wa kutumika, basi kitumike kwa manufaa ya nchi yetu na kuepuka wale wajanja kutumia nafasi kama ilivyo kwa maeneo ya baadhi ya sheria ambazo zinakuwa ziko kimya na watu wana-*take advantage*.

Nashukuru sana Mhe. Spika na ahsante sana.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia mambo mawili matatu kuhusu mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Kuweka Utekelezaji wa Majukumu na Uwezo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Haya.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyenijaalia jioni hii kuwa katika hali ya uhai na uzima na afya inaruhusu.

Vile vile nakushukuru wewe Mhe. Spika uliyenipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria.

Pia nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kutuletea mswada huu muhimu, ambao utakuwa ukombozi kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Nisiwe mchache wa shukrani nadhani kwa mashirikiano makubwa aliyotoa Mhe. Mwanasheria Mkuu, basi umekamilika tena ni mzuri sana.

Kabla ya kuendelea na mchango wangu naomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kuupitisha mswada huu, ili tuweze kuwa katika mazingira mazuri.

Mhe. Spika, mswada wa sheria ya kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni jambo zuri, kwa sababu ukiangalia katika nchi yetu hii kuna maeneo mengi yenye matatizo, lakini inapoanzishwa Sheria hii ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nadhani itasaidia sana.

Kwa kweli kuwepo katika Sheria ya Utumishi wa Umma ni jambo la wajibu hapa ulimwenguni, kwani sheria ndiyo inayopasa kutupa muongozo wa maisha ya mwanadamu na maslahi.

Mhe. Spika, sheria hii nikitoa mfano kuna migogoro mingi sana katika masuala ya ardhi, lakini sheria hii naamini itatusaidia.

Vile vile sheria hii itakuwa ni muongozo wa utawala wa sheria ndio inayostawisha utawala bora na kuimarika kwa misingi ya haki za binadamu.

Mhe. Spika, nimevutiwa sana na mswada huu hasa ukifungua kwenye kifungu cha 6(1) kuhusu uteuzi wa Naibu Mwanasheria Mkuu naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 6(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

1. "Kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu ambaye atateuliwa na Rais na hili sina pingamizi".

2. Mtu atafaa kuteuliwa Naibu Mwanasheria Mkuu iwapo:
   (a) ni Mzanzibari;
   (b) ana elimu isiyopungua shahada ya kwanza ya sheria kutoka taasisi ya elimu ya juu inayotambulika na chombo chenye mamlaka;
   (c) ana uzoefu katika fani ya sheria kwa angalau miaka saba; na
   (d) Mtu mwenye uadilifu.

Mhe. Spika, tunayo matumaini sana kama sheria hii na vigezo vilivyotajwa hapa hasa ukiangalia kifungu (d) kinavyozungumzia uadilifu. Kwa kweli hili ni jambo la kwanza kwamba yeyote atayeteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu kigezo hichi wakiangalie kuwa kina sifa zote za mswada huu, bila ya uadilifu hakuna jambo lolote litakalokuwa zuri. *(Makofi)*

Lakini haitoshi asiwe moga juu ya utendaji wa kazi zake, maana yake akiwa moga katika utendaji wa kazi zake ndio ule uadilifu unakuwa haupatikani kabisa. Kwa hivyo, Mhe. Spika tunaomba yeyote atayebahatika kuteuliwa kwenye nafasi hii basi wawe makini tena waadilifu na wala wasiwe na woga katika kufanya kazi zao, kwa sababu mambo wameyasomea na wanao uzoefu wa kutosha, basi wawe makini kweli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kama Mhe. Ismail Jussa Ladhu amezungumzia hapa kwamba ni mtu mmoja ambaye amejitolea kusema mambo ya uwazi kuhusiana na mambo ya nchi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, alichokizungumza Mhe. Mwanasheria huyu, mimi namuomba Mwenyezi Mungu kwamba nafasi hii huyu isimtoke na aendelee nayo na wakati mwengine achaguliwe tena kwa kujiamini kwake. Kwa maana kazi yoyote kama hukujiamini katika utendaji wake basi itakuwa dhaifu milele na milele, na wala haki haipatikani hata dakika. Lakini ikiwa sheria uliyoisomea na unakwenda kwa uaminifu na uadilifu, basi inakuwa jambo hili ni zuri sana. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu kwenye kifungu cha 5 cha mswada kuhusu Mwanasheria Mkuu, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 5 cha mswada kinaeleza hivi:-

1. "Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye Mkuu wa Ofisi;
2. Mwanasheria Mkuu atatekeleza kazi za jumla na maalum na kutimiza uwezo wake aliopewa na Katiba, Sheria hii na sheria nyengine husika".

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Mwanasheria Mkuu atakuwa na nafasi aliyopewa na Katiba kiuwezo. Kwa hivyo, tunamuomba kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba afanye kazi zake kwa mujibu wa taratibu pamoja na kujiamini kabisa kwa sababu uwezo amepewa na wala asibabaike kutokana na shindikizo la mtu na akifanya jambo kwa shindikizo la mtu, basi sheria hapo itakuwa imemshinda.

Lakini nadhani kama atakuwa muadilifu na wala hatokuwa moga basi atafanya kazi kwa uaminifu kabisa na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutapata zile haki zetu za kimsingi Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, kama ilivyoeleza na mswada wenyewe unavyojieleza mimi naamini kwamba mswada huu umekamilika vizuri sana na kama umekamilika, basi sina haja ya kuchangia mengi isipokuwa tunatoa baraka zetu tu kuonesha kwamba na sisi tumeuchangia.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nasema ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo na mimi nikaweza kuchangia Mswada huu muhimu wa Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwanza kabla ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuweza kufikiria jambo hili muhimu na kutayarisha mswada huu ambao hivi sasa uko mbele yetu, kwa ajili ya kuandaa sheria.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi ninapopata mswada wa sheria basi huwa ninafukuzia kwenye lile eneo la mwisho la madhumuni na sababu, kwa sababu huwezi kutunga sheria bila ya kuwa na sababu au huwezi kufanya marekebisho ya sheria bila ya kuwa na sababu ya kufanya hivyo.

Kwa maana hiyo, ili niuelewe vizuri mswada wa sheria basi moja kwa moja naelekea kwenye maeneo yanayozungumzia madhumuni na sababu ya kutungwa sheria hii.

Mhe. Spika, sheria hii Mhe. Waziri ametueleza sababu nyingi na moja miongoni mwa sababu ambayo ni kubwa ni kutokana na kwamba Ofisi hii ya Mwanasheria Mkuu haina sheria, jambo ambalo baadhi ya wakati linatupa shida.

Lakini katika historia yangu ya kupitisha miswada ya sheria kwa muda huu wa miaka saba na kidogo, basi sheria hii ndio ya kwanza iliyoeleza madhumuni mengine kuliko miswada mengine yoyote na mimi nampongeza sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Uzoefu wa miswada ya sheria hapa wakati mwengine Mawaziri huwa wanatueleza tu sababu mstari mmoja au miwili na halafu wakarejea vile vifungu ambavyo tayari tunavyo hapa. Kwa mfano, kifungu cha kwanza sehemu ya kwanza inasema hivi, kifungu cha pili sehemu ya pili, kwa hiyo anarejea yale ambayo tunayo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri kupitia kwako Mhe. Spika, wanapotuandalia miswada hii ya sheria basi wafuate mfumo huu, ambapo Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi ya kujua kwa kina madhumuni na sababu ya kutungwa kwa sheria husika.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba pengine hawa watu wa Ofisi ya Mwanasheria wanajipendelea na wanajipendelea hata uandishi wa mswada wenyewe uko tofauti na miswada mengine ambayo tunaletewa hapa. Kwa kweli mswada huu umeandikwa vizuri, unaeleweka na wala hakusukumwa na ndio maana hatukupata tabu. *(Makofi)*

Lakini jambo la kufurahisha zaidi Mhe. Spika, katika sheria hii ya Ofisi ya Mwanasheria kuna eneo ambalo linaeleza kwamba sasa kutakuwa na Sera ya Uandishi wa Sheria na miongozo namna miswada yetu ya sheria iwe. Nadhani tutakapoipitisha sheria hii tutakuwa sasa hatupati tabu, kwa sababu tutakuwa na *format* ya aina moja ambayo Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wameshaizoea na wala hakuna leo huu umeandikwa hivi na kesho umeandikwa vile na wala hatuelewi tunasoma nini, kwa hiyo hii itasaidia.

Kwa kweli Mhe. Spika, mswada tuliokuwa tukiujadili juzi wa Wizara ya Ardhi uliandikwa vibaya sana na ndio maana ulikuwa haueleweki, kwa sababu cha huku kimechukuliwa na kuelekea huku na cha kule kimechukuliwa

kimewekwa huku na ndio tulikuwa tukipata tabu. Lakini kwa mswada kama huu hakuna tatizo umeandikwa vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, moja kati ya sababu Mhe. Waziri ameeleza ni umuhimu wa kutunga sheria baada ya Ofisi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutokuwa na sheria ya kuiongoza na ameeleza sababu nyingi.

Namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba afanye utafiti wa kutosha juu ya maeneo ambayo yanayohitaji kutungiwa sheria, kwa sababu si hii tu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambayo muda mrefu haijatungiwa sheria ya kuiongoza. Kwa kweli yapo mambo mengi ambayo yanahitaji kutungiwa sheria ambayo ni dhahiri hata muongozo wake tunashindwa kuuelewa.

Kwa mfano, katika kipindi hichi nchi yetu imeingia kwenye mabadiliko makubwa ya Muundo wa Serikali, ambapo sasa kwa mujibu wa Katiba tumekuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambayo imetajwa kwenye Katiba na vimetajwa baadhi ya vifungu vya Katiba.

Mhe. Spika, mimi naona kwa mtazamo wangu kuna haja ya kutunga sheria juu ya namna ya utekelezaji wa serikali hiyo, kama hatutatunga sheria basi siku za baadae tunaweza kuwa na matatizo kwenye utekelezaji na zaidi ukizingatia kwamba serikali hii inaongozwa na pande mbili, yaani chama kinachotawala na chama cha pili kinachoshinda. Sasa kama hatutatunga sheria juu ya utekelezaji wa serikali hiyo, tukaiacha kama Katiba tu ilivyo baadae tunaweza tukapata matatizo.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba aiangalie suala hili pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na kuona umuhimu wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mswada huu wa sheria kifungu cha 6(1) ambacho kinazungumzia kuhusu uteuzi wa Naibu Mwanasheria Mkuu, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 6(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

"Kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu, ambaye atateuliwa na Rais".

Jambo hili ni jema na kwa sababu Mwanasheria anayo kazi au jukumu kubwa, lazima awepo msaidizi wa kumsaidia Naibu Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, Naibu Mwanasheria Mkuu huyu ataweza kumsaidia Mwanasheria katika utekelezaji wa shughuli zake na kuwemo kwenye sheria au kulazimisha kwamba sheria hii awepo ni jambo muhimu.

Mhe. Spika, jana tulipokuwa tukipitisha sheria hapa, ambayo ilikuwa inasema kwamba ikiwa Rais ataona umuhimu wa kuwepo Naibu Mkurugenzi basi atateua tulipokuwa tukipitisha sheria ya Mkurugenzi Mkuu, nilisema kwamba ikiwa ipo haja ya kuwepo Naibu Mkurugenzi Mkuu basi namuachia Rais.

Lakini sheria hii imezungumza moja kwa moja kwamba ni lazima awepo Naibu Mwanasheria Mkuu kutokana na umuhimu wa jambo lenyewe, kwa hiyo mimi nalipongeza jambo hili.

Vile vile kwenye kifungu cha 7 kinazungumzia kazi za Naibu Mwanasheria Mkuu ambapo kifungu cha 7(2), naomba nikinukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 7(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

2 "Isipokuwa kama Rais ataamua vyenginevyo pale ambapo Mwanasheria Mkuu hawezi kutekeleza wajibu wake kwa muda na kwa sababu ya kutowepo ofisini kwa ugonjwa au sababu nyenginezo Naibu Mwanasheria Mkuu atatekeleza kazi na kutumia uwezo wake wa Mwanasheria Mkuu.

Isipokuwa kwamba na kwa ajili ya kuondoa shaka masharti ya kifungu hichi hayatatafsiriwa kuwa yanamruhusu Naibu Mwanasheria Mkuu kumwakilisha Mwanasheria Mkuu katika vyombo ambavyo ujumbe wa Mwanasheria Mkuu katika vyombo hivyo umewekwa na Katiba".

Mhe. Spika, jambo hili ambalo limezungumzwa humu kwenye sheria si jambo ambalo halijaweza kutokea katika nchi yetu. Jambo hili limewahi kutokea ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipatwa na maradhi na akashindwa kufanya shughuli zake kutokana na maradhi na hili limetokea. Kwa kweli Mhe. Spika, kipindi ambacho Mwanasheria Mkuu yule aliyepita alishindwa kufanya kazi zake Baraza lako la Wawakilishi na wakati ule ukiwa Spika tulipata tabu sana.

Baraza lilikuwa linakwenda kama chombo kilichokosa nahodha, kwa sababu chombo hichi Mhe. Spika ni chombo cha kutunga sheria kilihitaji au kinahitaji mtu wa aina hii tena sana. Kwa hivyo, kukosekana mtu wa aina hii maana yake chombo hichi kitakuwa kinakwenda bila ya kuwa na Mshauri wa Sheria au hakuna mtu mwenye uwezo wa kutoa ufafanuzi wa kisheria na tutakuwa tunakwenda. Kwa maana hiyo, pale ndipo tulipoona umuhimu wa kuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu.

Sasa sheria hii kifungu cha 7(2) kimeeleza kazi za Naibu Mwanasheria Mkuu pale ambapo Mwanasheria anapopata dharura kama zilivyotajwa kwa mujibu wa kifungu cha 2. Lakini tumesahau kwamba Mwanasheria mbali ya shughuli zake za ofisini tunamuhitaji humu awemo kwenye chombo hichi kwa ajili ya kutusaidia.

Kwa hivyo, hebu tujiulize je shughuli hizo ambazo anahitajika hapa Naibu Mwanasheria Mkuu ataweza kuja huku kufanya shughuli hizi za kutusaidia katika utungaji pamoja na mambo ya ushauri wa kisheria, twabaan utaona kwamba haiwezekani.

Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo hili tayari limeshawahi kutukuta basi naomba sheria hii ifanye mazingira ya kumuwezesha Naibu Mwanasheria Mkuu aweze kuingia kwenye chombo hichi, kwa ajili ya kusaidiana na Mwanasheria kama itawezekana na hata kama ikibidi kubadilisha Katiba basi tubadilishe Katiba kwa sababu Katiba si Msahafu, kwa sababu haya mambo tayari yameshawahi kutokea na wala sio jambo la kufikiriwa tu ni mambo ambayo yametokea na tuliona umuhimu wa jambo hili.

Kwa hivyo, hata ikibidi kubadilisha Katiba baadae juu ya Naibu Mwanasheria naye kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi hapa, ili asaidiane na Mwanasheria ni jambo muhimu.

Mhe. Spika, kifungu cha 8 kinazungumzia muundo wa ofisi ambapo kifungu cha 8(2), naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 8(2) na (3) cha mswada kinaeleza hivi:-

2 “Iwapo Idara zitaanzishwa, uteuzi wa wakuu wa Idara hizo utafanywa kwa mujibu wa sheria husika za utumishi wa umma;

3. Iwapo Mwanasheria Mkuu ataanzisha vitengo ama chini ya Idara zilizoanzishwa chini ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki au bila ya kuwepo Idara atateua wakuu wa vitengo kwa masharti kama anavyoona inafaa na kwa mujibu wa muundo wa Utumishi wa Ofisi”.

Mhe. Spika, hapa mswada wa sheria imezungumzia mambo mawili kuwepo kwa idara au kutowepo. Lakini ninachotaka kusema Mhe. Spika hapa sisi tunatunga sheria kama uamuzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu basi kuwe na Wakuu wa idara sheria iseme na kama tukiona kwamba hakuna idara na wakuu wa vitengo pia sheria iseme kama kutakuwa na wakuu wa vitengo, hivi tunamsubiri nani atuamulie ni hii Ofisi ya Utumishi wa Umma?

Mimi nadhani hapa sheria hii ieleze kwamba kutakuwa na Wakuu wa Idara kama watatu na idara zenyewe zitajwe. Sasa suala la utaratibu na mipango na namna yenyewe idara zitavyokuwa tutaiachia yenyewe Idara ya Utumishi. Kwa kweli hatuwezi kutunga sheria ambayo inakhiyarisha, isipokuwa tuweke moja kwa moja na kama tunahisi kwamba jambo hili kuziweka Idara katika Ofisi hii si jambo muafaka basi tuseme tu kwamba tutakuwa na vitengo vya Idara na Mhe. Mwanasheria ataanzisha vitengo chini ya Idara zinazoanzishwa. Kwa sababu sisi tunatakiwa tufute sheria ambazo zimetungwa na kila mmoja aelekezwe na sheria kwa hivyo hatuwezi kuakhirisha hapa ama wawepo wakuu wa Idara ama wawemo Wakuu wa Vitengo kwa mujibu wa sheria. Tuchague moja ama wakuu wa Idara au Wakuu wa Vitengo ili taasisi inayohusika basi ieleze namna ya Idara hizo zitakavyokuwa au vitengo hivyo vitakavyokua.

Mhe. Spika, kifungu cha 16 kinazungumzia uwezo wa Mwanasheria Mkuu na Ofisi, kifungu hiki Mhe. Spika, kimeeleza mambo mengi lakini moja ambalo nataka kulizungumzia na ni jambo muhimu na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwepo kwa jambo hili kama nilivyotangulia kusema kifungu cha 16(a) kuandaa mapendekezo ya sheria kuwa katika miswada kwa ajili ya kutungwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na kutayarisha hati zote za kisheria na zisizokuwa za kisheria. Hili ni jambo muhimu Mhe. Spika, ambayo nchi yetu sasa kwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tutakuwa na taratibu zile ambazo ziko sawa kuliko ilivyo sasa. Kumekuwa hakuna utaratibu kila Wizara inajifanyia inavyotaka, kwa hivyo hili litasaidia kuona hati za serikali miswada ya serikali inaandikwa na Ofisi moja tunakuwa na *format* moja. Kwa hivyo katika hili tutakuwa hatuna mashaka.

Lakini hata kifungu cha 19 cha sheria hii kifungu kidogo cha (3) ambacho kinasema, 'Mwanasheria Mkuu anaweza baada ya kushauriana na Mamlaka ya Utumishi wa Umma husika kupendekeza muundo wa utumishi na maofisa ambao sheria hii inatumika kwa ajili ya kudumisha maendeleo ya kitaaluma yenye uwiano katika kada'. Muundo wa Utumishi ni muhimu na kwa sababu tunapoandalia muundo wa utumishi watu wetu watakuwa wanapata nafasi ya kuona umuhimu wa shughuli zao kuliko kuacha tu kama ilivyo, hili jambo ni muhimu na muhimu kuwemo katika sheria ili kuona kwamba hawa maofisa wa sheria watakaokuwepo katika Ofisi hii au katika Ofisi nyengine za umma basi wanakuwa na muundo maalum ambao utawawezesha kujitambua namna gani walivyo na maslahi yao yakoje. Kwa hivyo hilo ni jambo muhimu sana na ni jambo ambalo linahitaji kuwepo katika maeneo mengi ya serikali.

Mhe. Spika, mswada huu umeeleza mambo mengi ni mswada ulioandikika, umeandikwa kitaalamu una manufaa makubwa umeeleza mambo mengi masuala yanayohusu mikataba, kwamba sasa mikataba itakuwa inaandikwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na niombe Mhe. Spika, nchi yetu tayari inayo mikataba tumeshafunga mikataba mingi basi sheria hii inapopita mswada huu utakapopita na kuwa sheria basi niiombe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu basi ipitie mikataba yote na ile inayohitaji kufanyiwa marekebisho basi ifanyiwe marekebisho. Asubuhi hapa tulikuwa tunazungumzia suala la uwanja wa ndege sijui uko hivi, tuko hivi pale ni taratibu tu za mikataba zimekosekana, zile lugha nyengine tunazoambizana uwanja uko hivi, sijui pesa ziko hivi, sijui hivi hivi, ile ni lugha tu ya kuambizana ambizana tu. Lakini tatizo kubwa la ujenzi wa uwanja ule ni mikataba ya sheria hayo mengine yote tunaambizana tu hapa. Na kwa sababu Mhe. Spika, mara nyingi sisi tatizo letu linakuwa pesa kila wakati hatuna fedha lakini hata pale pesa zinapopatikana napo linakuwa tatizo. Kwa sababu pesa kwa ajili ya ujenzi wa uwanja ule zilikuwepo. Wenzetu ndugu zetu wa Jamhuri ya Watu wa China tulipowaomba dola bilioni 70 walitupa hizi kajengeni uwanja sasa tatizo liko wapi. Pesa tunazo, uwanja tunao, wataalamu wapo tatizo nini?

Mimi nadhani Mhe. Spika, ni tatizo la mikataba ambayo tunaingia iwe mikataba ya kimataifa au mikataba yetu ya ndani. Kwa hivyo suala la mikataba hili sasa kuwekwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itaisaidia serikali kuweza sasa kutekeleza mambo yake bila ya matatizo. Na ameeleza hapa kwamba madhumuni mengine makubwa ya kuandika mswada huu wa sheria au ya kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria kisheria ni pale ambapo Mwanasheria anatoa ushauri wa kisheria lakini mwanasheria mwengine tu katika taasisi nyengine anapingana nao tu na yeye Mwanasheria anaelekeza vyenginevyo, lakini kupitishwa kwa sheria hii basi sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ushauri wake anaoutoa utakuwa ndio *final* ama Rais labda aagize vyenginevyo kwa sababu yeye ndiye bwana mkubwa au mahkama. Lakini huko nyuma ilikuwa tu kila mmoja mwanasheria anaweza kuandaa mkataba basi mkataba ule ukachukuliwa ukapelekwa Wizarani watu wakabadilisha wanavyotaka, hakuna sheria jambo ambalo limetufikisha pahala pagumu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu wa kuanzishwa kwa usimamizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kisheria na nimuombe Mwanasheria aangalie na maeneo mengine ambayo yanahitaji kuanzishwa sheria yasikae tu yakawa yananingin'ia hayana kitu ambacho kimejishika. Na kwa sababu tunapokuwa na sheria ndizo zitakazotuongoza yanapotokea matatizo hata tukifikishana mahkamani, mahkama sasa itabidi iangalie sheria inasemaji. Sasa kama hakuna sheria maana yake hata wenzetu wa mahkama watakuwa hawana kitu kinachowaongoza katika kutatua jambo lile. Kwa hivyo tuangalie maeneo yote sio Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, yale yanayohitaji kuanzishiwa sheria basi tuyatungie sheria ili iwe ndio muongozo wa mambo yale.

Mhe. Spika, baada ya maelezo mafupi naunga mkono mswada huu wa sheria na kwa niaba ya wananchi wangu tunakubaliana nao kwa asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, ninakushukuru umeniona ninahangaika hangaika leo Mhe. Spika, mimi nina furaha kubwa sana watu wengi wananiambia niandike kitabu, niandike historia, lakini nilikuja Ofisini kwako

nikakwambia Mheshimiwa mimi nataka kuandika kitu kuhusu Baraza, ukanambia *wallahi* si jambo baya lakini nifanye utafiti. Lakini sasa nimebadilisha mawazo sasa kama utaniruhusu niandike historia yako na haya ninayosema ninayasema ndani ya moyo wangu.

Mhe. Spika, leo ni siku ya furaha kubwa kwako wewe, si wengi wanajua kwa nini leo siku ya furaha. Mhe. Spika, wewe mwaka 1992 ulibahatika kuchaguliwa kwenye Tume ya Rais kuuliza wananchi mfumo gani serikali moja au mbili, mfumo wa vyama vingi na ulikuwa kwenye Tume ile. Historia watu wakipenda wasipende Mhe. Kificho ulikuwa kwenye Tume ile lakini tume ile ulichaguliwa kuwa ni Mjumbe wa Baraza Wawakishi sio kama mtu binafsi, ukafanya kazi ile leo Mhe. Kificho Mhe. Spika, nisamehe sijui kama kumnukuu mtu *hansard* yake inataka ku-*copyright* lakini kama inataka *copyright* mruhusu kama haitaki kibaraza niruhusu kidogo nikunukuu kwa kuthibitisha kama unastahiki kuandikwa katika historia ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ninayo hapa *hansard* yako ndogo sana ya mwaka 1992 lakini ulisema maneno mazito sana ulisema una-*observation* unasema kwa hivyo *observation* ya pili inaeleza kwamba pande zote mbili za wataka vyama vingi na chama kimoja wanakubaliana suala moja muhimu la usalama wa nchi hii, umoja wa nchi hii, amani na utulivu wa nchi hii na wanasema hilo ni la kwanza kabisa. Mhe. Spika, wewe unasema kwamba hata maendeleo yawe mazuri kiasi gani kama hakuna amani, usalama, utulivu pamoja na umoja basi maendeleo hayo hayana haja nayo. Hiyo ni *observation* yako. Baraza hili tukufu leo lina miaka miwili na nusu umechaguliwa tena kuwa Spika na umeongoza Baraza la mwanzo la aina yake lenye misingi hiyo ambayo ulifanya *observation* mwaka 1992.

Mhe. Salmin Awadh anasema serikali hii ni serikali ya mapinduzi yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Iko haja kuwepo na sheria au taratibu za serikali kuendesha nakubaliana naye moja kwa moja na ninawafiki, mimi nilikuwa ndie Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi kushughulikia suala la *referendum* na tukaenda Ulaya tukajifunza na ripoti yetu tukaandika lazima iwepo sheria, utaratibu namna gani kuiendesha serikali ya Umoja wa Kitaifa nakubaliana nae na ripoti tumeikabidhi serikalini. Mhe. Spika, naomba ufuatilie hilo.

Sasa Mhe. Spika, furaha yangu ya pili ambayo na wewe leo Mhe. Spika, ni yako. Mhe. umesema hivi, Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa ndio amekuwa Mwanasheria Mkuu kwa hivyo yeye ndio ameingia kwa sababu ya Wizara hiyo. Lakini ingekuwa Mwanasheria Mkuu wake haujachanganywa na Waziri wa Tawala za Mikoa basi katika Baraza hili tungekuwa hatuna rasmi Mwanasheria katika shughuli zote. Na huo ungekuwa ni upungufu mkubwa sana. Mhe. Spika, chombo hiki kazi yake kubwa au moja kati ya kazi yake kubwa ni kutunga sheria za nchi hii. Ni kwa kweli ni kinyume kabisa kuona kwamba sisi tunatengeneza hizo sheria si wataalamu wa sheria. Tunaweza kwa kiasi kikubwa tukapendekeza mambo ambayo yapo kinyume na sheria kiulimwengu na pengine tunaweza tukapendekeza mambo ambayo kinyume na Katiba wakati Katiba ndio sheria kuu.

Kwa hivyo kumuingiza Mwanasheria Mkuu humu kwa kweli kunasaidia sana kujaribu kwa kiasi kikubwa sana kuhakikisha kwamba mambo yetu yote yatakuwa yanakwenda kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Isipokuwa mimi kwenye kifungu hicho ambacho ni kifungu cha saba cha marekebisho ya mswada huu nilikuwa na maoni ya nyongeza kidogo kuliko vile ambavyo imeainishwa hapa.
Mhe. Spika, kwa sababu umuhimu wa wanasheria mimi nadhani hii nafasi moja ya mwanasheria peke yake ni ndogo haitoshi. Serikali inakwenda kwa mujibu wa tararatibu za kisheria, na serikali ina mambo mengi sana Mhe. Spika, ambayo yote yanatakiwa yafuatane na sheria ambayo ni Katiba. Sasa kwa mambo yote ambayo yanaendelea wakati wa majadiliano ndani ya Baraza hilo tukufu hili kwa mfano mswada huu itabidi mwanasheria huyu ana kazi kubwa sana ya kuona kila analozungumza na Mjumbe wake awe analingana hapa na pale kama nimeliona na taratibu na sheria nyengine zilivyo, ningesema kwa kweli nafasi ya wanasheria wakuu lakini ingekuwa nafasi nyengine kama nne hivi zikawa nafasi 5 za wanasheria ndani ya Baraza hili. Leo Mhe. Spika, siku ya furaha kwako ndani ya Baraza hili kuna wanasheria 4 na wewe mwenyewe ukiwa ni wa tano kwa ile *dream* yako ime-*come true* leo umekaa juu ya kiti ndani ya Baraza mna Wajumbe wane na wewe mwenyewe ni mwanasheria, unaona mbali Mhe. Spika, leo ni siku yako ya furaha historia imetimia.

Sasa Mheshimiwa nataka niende katika mswada. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni Ofisi muhimu sana. Leo si kitu kipya lakini kitu kipya kwa hapa, kwa Tanzania kwa Kenya na Uganda. Mwanasheria Mkuu ni mwanasiasa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema Mwanasheria Mkuu atateuliwa kutokana miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa za kufanya kazi wakili au watu wenye sifa za kusajiliwa. Mwanasheria Mkuu atakuwa Mjumbe wa Baraza la Mawaziri Mbunge ni mwanasiasa.

Katiba ya Kenya ya juzi ambayo inasema, "*They shall….. the Attorney General shall be nominated by the president with approval of National Assembly. Attorney General shall have authority with leave of court. Attorney General shall promote, protect and uphold rule of law and defend public interest. The power of Attorney General may exercise a person or subordination"* hii ya Kenya.

Katiba ya Zanzibar ya 1995 kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ambaye ni Mzanzibari na ambaye Rais atamteua. Mwanasheria Mkuu atakuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutokana na wadhifa wake na atashika ujumbe huo mpaka uteuzi wake utakapofutwa na Rais au mara tu kabla ya Rais Mteule kushika nafasi.

Kwa hivyo nafasi ya Mwanasheria Mkuu ni nafasi muhimu sana. Leo tunaweka historia nataka nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akiwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kukubali kuleta sheria ya kuweka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kisheria si kikatiba nataka nimpongeze na mpelekee salamu zetu aitie saini sheria hii na ameweka historia. Leo Mhe. Spika, Mwanasheria Mkuu wa kwanza wa Ofisi yake ilikuwa mwaka 1914 leo mwaka 2013 ni miaka 99 tunaweka historia Zanzibar na wewe ukiwa Spika, unapitisha sheria hiyo ambayo kwa mara ya mwanzo kwa historia unaweka kisheria Mwanasheria baada ya miaka 99 *may God bless you*. Mwenyezi Mungu akupe maisha marefu, akupe hekima na busara na sisi unaotuongoza. Leo ni siku ya furaha tunaweka historia.

Lakini nini maana yake unapoweka kisheria Mwanasheria Mkuu, maana yake unataka kutekeleza haki, usawa sheria bila ya ubaguzi bila ya kuoneana, sheria ifanye kazi. Kwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi leo tunapitisha azimio kubwa sana na historia itatukumbuka tumepitisha sheria tuipitishe kwa kauli moja kumpa nguvu Mwanasheria Mkuu kwa sheria hii.

Mhe. Spika, mswada huu mimi nilibahatika kualikwa kwenye semina na sijapata mimi kuona mswada una madhumuni *page* sita ila huu. Ni madhumuni tu umeandikwa uzuri, na ndio maana kila mtu anaunga mkono unakwenda vizuri lakini tumeweka historia. Lakini ndani yake Mhe. Spika, tuwakumbuke kihistoria wenzetu Mhe. Spika, wamekuwa nchi hii wengi humu ndani ni watoto wa Mapinduzi, wamezaliwa mapinduzi, wamekuwa wakubwa, mapinduzi maana yake kuwa mtu mzima wa miaka 18. Kwa hivyo wale ambao wana miaka 68 lakini kidogo sana humu ndani sitini na nane na chini. Kwa hivyo wengi ni vijana lakini tumetoka katika mapinduzi, leo ni miaka 49 tumepita hatua 3. Tumeanza na Baraza la Mapinduzi kwa miaka 21 tukaingia Baraza la Wawakilishi.

Baraza la Mapinduzi limekuwa na wanasheria, wa kwanza Wolfgong Dourado marehemu historia lazima leo tumtamke. Wa pili Bashiri Swanzi wa tatu Damian Lubuva. Hawa walikuwa wanasheria ndani ya Baraza la Mapinduzi. Baraza la Wawakilishi wa kwanza kabisa Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni yule pale.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary Mhe. Spika, ni mtu mwenye bahati sana. Mhe. Abuu ndio karani wa mwanzo wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Abuu ndiye Mwanasheria aliyetunga hii sheria ya mwaka 1984 leo Mhe. Abuu ni Waziri wa Sheria na Katiba na yeye ndiye sheria kaileta Mhe. Abuu hongera sana.

Wa pili Mhe. Hamid Mahmoud ambaye amefanya kazi nzuri amestaafu kama Jaji Mkuu. Muelezeni, marehemu Saleh Abdalla Dahoma, Ali Mohammed Omar huyu alikuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi akawa Mwanasheria Mkuu, Iddi Pandu Hassan tumekuwa naye mara mbili akiwa Mwanasheria Mkuu ni mwenzetu, kafanya kazi nzuri na leo kamtaja Mheshimiwa na sijui kama tunamtunza tunamtazama, lakini anastahiki kila sifa kwa sababu vuguvugu lote la Baraza hili kapambana nalo Iddi Pandu.

Mwengine Omar Makungu na leo yuko Othman Masoud. Hawa jumla yao 11 sawa sawa na timu ya mpira, kiti cha mfalme wa Lebanon kimeandikwa nyuma ya kiti chake kama asingeondoka, usingekaa, kama asingeondoka Mhe.Idriss Abdulwakil asingekaa Mhe. Ali Khamis, usingekaa Mhe. Spika, leo lakini na wewe utaondoka. Lakini utaondokaje, utaondoka kwa heshima kama hizi tunazoeleza. Historia utaiacha, kwa hivyo lazima tuheshimu wenzetu ambao wamepita na wamefanya kazi, tujenge *culture* hiyo ya kuheshimu sio tukitoka basi basi, hapana wamefanya kazi tuwaheshimu.

Jengine Mhe. Spika, watu wanasema mwanasheria Mkuu anasema sana, anajibu sana nataka nimsemee Mwanasheria Mkuu ni mwanasiasa. Katiba inasema, Baraza la Mawaziri wakitajwa na yeye yumo nitatoa mfano kuthibitisha hilo.

Kikao cha LEGICO cha mwaka 1952 hii hapa *hansard* yake lakini nimetaipu kwa sababu iko *so dark* anasema hivi, nataka kuithibitisha kama ni mwanasiasa, Bwana *Attorney General* alieleza Baraza bili ambazo zinatakiwa ziwe ni bili 17, lakini leo hapa ninazieleza bili *Gazette ana report hansard* bili mbili, bili zenyewe ni hizi:

- Kubadilisha sheria inayoandamana na Ulevi wa kienyeji kama vile tende, pombe, tangara, tende ya embe na kadhalika.

Mhe. Ameir Tajo alitoa rai yake kuwa inafaa sana kwamba wakosa wa sheria hiyo wapate adhabu nzito ili yapate kukoma mambo hayo machafu ya ulevi, yanasababisha watu kuuwana kwenye mutukari, mutukari kupinduka au kugongana, kumuuwa mtu, sasa Mwanasheria Mkuu anajibu.

Mwanasheria Mkuu sasa anasema, furaha kubwa anayo lakini adabu italingana na sheria iliyowekwa na Mahkama. Sasa nini lakuonesha kwa kuwa si jambo jipya, si jambo geni ni jambo la sawa Mwanasheria Mkuu kusema ni mwana siasa, kujibu na kutoa ufafanuzi. Mhe. AG anafanya wajibu wake kwa sababu ni kazi yake kusaidia serikali, kusaidia Wawakilishi na nimechukua hii *hansard* ya mwaka 1952 LEGICO**,** si wengi wanaomjua Sheikh Ameir Tajo humu, humu ndani Mhe. Spika, wengine masheikh na wengine maprofesa humu, humu ndani maprofesa utawapata, masheikh, maulamaa, mufti; humu ndani wanaingia wanasiasa kazi yao siasa, kazi yao kusema na kutetea haki za wananchi na serikali yao. Kwa hivyo, sisi sote tuna jukumu la kuendeleza amani na utulivu.

Vile vile nataka niombe wenzangu Wawakilishi upande wa vyama vyetu vya siasa tujiepushe na lugha ambazo zitaharibu huu mti tulioupanda, tuepukane na lugha mbaya, chafu, tujenge nchi kwa manufaa yetu tutengeneze mambo kwa amani na utulivu na wala tusitetee maovu na uchafu.

Mhe. Spika, niliona nitie ubani katika mazungumzo haya na leo ni siku ya furaha hasa kwako uliyoyafikiria, uliyoyasema leo yametimia. Liko moja humu sijalisema kwa sababu sio siku yake hapa leo ikifika siku yake nitalisema jengine kubwa sana lakini hilo kwa laini nyengine, bali kwa Mwanasheria leo una wanasheria saba ndani ya Baraza la Wawakilishi wafanyakazi haijapata kutokezea, chini ya utawala wako hongera Mheshimiwa. Sikusifu kwa kutaka chochote nakusifu kwa haki yako na ukweli.

Jengine unajua uhusiano wangu mimi na wewe sisi marafiki, nimekupa ninavyovipenda seuze vyengine. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi na wewe tunaelewana na ni ndugu. Mhe. Spika, naunga mkono ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nichangie mswada huu. Mimi nitachangia katika kifungu cha 4(2), kifungu hiki Mhe. Spika, nilikuwa naomba ufafanuzi kwa Mhe. Waziri. Kifungu kinasema, Ofisi itakuwa taasisi huru na yenye mamlaka ya kujiendesha ndani ya utumishi wa umma Zanzibar. Sasa nataka ufafanuzi katika kifungu hiki kuhusu suala la uajiri kwa wafanyakazi pamoja na maslahi yake. Maana yake ni kwamba taasisi hii itaajiri na itafanya mambo ya mishahara kwa wafanyakazi wake? Hili nataka ufafanuzi.

Halafu kifungu nambari 5(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa kiongozi wa mawakili. Hapa pia nataka ufafanuzi kwa sababu kifungu hakijaeleza wazi ni mawakili wa aina gani. Kwa sababu kuna mawakili wa binafsi na mawakili wa serikali kwa hivyo na hapa nataka ufafanuzi nijue kama ni mawakili wa serikali au wa binafsi.

Hapo hapo wakati serikali inaleta mswada huu kusimamia Wanasheria wake na Maafisa wa sheria kwa upande wa mawakili binafsi ambao wanatumia sheria ile ya zamani sura ya 29 na ambayo imepitwa na wakati je, ni lini sheria hiyo italetwa hapa kufanyiwa marekebisho? Nitachangia tena katika kifungu cha 28.

Mhe. Spika, kifungu cha 28 kinatoa kinga kwa Maafisa wa Sheria, hiki kifungu ni kizuri lakini kinaonekana kutengana na ile sheria ya mwenendo wa madai ya serikali ambayo Mwanasheria wa serikali kawekewa adhabu iwapo atashindwa kesi. Nahisi kifungu hiki kifutwe kutokana na sheria hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kuchangia huu mswada wa kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, lakini vile vile na kuweka utekelezaji wa majukumu yake na uwezo wa kuipa ofisi yake au na yeye mwenyewe katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, wenzangu wameshatoa pongezi nyingi na ingawa unatukataza kurejea rejea, lakini wakati mwengine Mhe. Spika, itabidi utuwie radhi kwa sababu mtu anapofanya vizuri ni haki yake kushukuriwa. Kwa hivyo, mswada

huu kwa kweli umekuja katika wakati muwafaka na umekuja katika wakati muwafaka kwa sababu sasa hivi hatutaki tena kufanya kazi kwa mazowea tunataka kufanya kwa kufuata sheria. Mwanasheria Mkuu ofisi yake sio kama ilikuwa haipo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilikuwepo na wanasheria wakuu kama walivyosema wenzangu wamepita wengi, lakini bado ilikuwa hatujaipa mashiko na meno ya kuweza kufanya kazi zake na kusimamia wengine waliokuwa chini yake.

Mhe. Spika, mswada huu sasa utaiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu lakini pamoja na Mwanasheria Mkuu kuweza sasa kusimamia shughuli zote za kisheria ndani ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ofisi hii ina dhima kubwa sana kwa nchi yetu na maslahi ya nchi yetu pamoja na wananchi wetu. Mhe. Spika, serikali inaposhtakiwa anakuwa hashtakiwi mtu isipokuwa inashtakiwa serikali na ikishtakiwa serikali ina maana ameshtakiwa Mwanasheria Mkuu. Sasa kuanzishwa au kupitishwa kwa sheria hii itampa sasa Mwanasheria Mkuu kuweza kudhibiti mambo mengi ndani ya serikali yetu ili serikali isije ikafika pahala ikashtakiwa. Sasa hili ni jukumu kubwa sana kwa ofisi yetu hii ya Mwansheria Mkuu na tunaamini wataweza kuyatekeleza kama tutakavyoipitisha hii sheria na nguvu tutakazoweza kuwapa.

Lakini la pili Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu, kwa sababu mswada huu najua ni jitihada zao ndio ukaweza kufikia katika *staged* hii tuliokuwanayo. Lakini kubwa zaidi Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa usikivu wale, lakini vile vile kujali mamlaka ya chombo chako kitukufu vha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kutokana na uzito wa mswada huu aliamua kwa makusudi kutuita wenyeviti wa kamati kuja kuuleta mbele yetu mswada huu tukaujadili, tukaufahamu, lakini vile vile na sisi kuweza kutoa maoni yetu. Mhe. Spika, nataka nikuthibitishie ile kazi uliyotutuma ya kutengeneza utaratibu ya kuwa na *autonomy* ya Baraza pamoja na kwamba bado sheria haijaja mbele yako au haujaja mswada wa sheria mbele yako, lakini tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba tayari wameanza kuruhusu *autonomy* ya Baraza au mamlaka ya Baraza kuanza kujitegemea na kuweza kusimamia shughuli zake.

Mhe. Spika, mfano huu unakuja moja kwa moja katika marekebisho ya kifungu cha 2(3) cha mswada huu. Mhe. Spika, kwa kuwa taa zetu zinawaka na kuzima na macho yangu kipindi hiki kidogo yamekuwa na giza sasa sitotaka kukisoma kifungu lakini nitazungumza maudhui ambayo nimekusudia.

Mswada huu Mhe. Spika, ulikuwa unampa mamlaka Mwanasheria Mkuu kuweza kuwasimamia Wanasheria wote isipokuwa wale wa Ofisi ya *DPP* na wengine lakini ilikuwa mpaka wale wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, baada ya kukaa katika kamati tukajadili na tukajaribu kutoa na uzoefu wa Mabunge mengine na kwa bahati nzuri Mhe. Mwanasheria Mkuu na yeye alituunga mkono katika ile ziara uliyotutuma kwenda kujifunza ni namna gani Mabunge yanavyotakiwa kufanya shughuli zake. Kwa kweli tunamshukuru sana, baada ya kutoa uzoefu na kutoa mifano mbali mbali alikubali kuiachia Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi kiuweza kuwahudumia watendaji wake wakiwemo Wanasheria wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo hili Mhe. Spika, kwa niaba yako maana yake hili ilikuwa usimame wewe utoe shukurani, lakini kwa bahati huko uliko hupati nafasi ya kuchangia sasa sisi wenyeviti wako uliotutuma hizo kazi basi tunatoa shukurani kwa niaba yako kwamba serikali kweli sasa hivi imekubali na imetia nia kweli ya kuweza kusimamia utawala bora na katika kuwekao ile *separation of power*. Kwa hivyo, Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu tunakushukuruni sana na tunaamini hata huko mbele tutakakokwenda katika kuja kutengeneza ile sheria yetu naamini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia Waziri wa Katiba na Sheria watatusaidia sana kuweza kutengeneza sheria nzuri ambayo italeta ufanisi katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo ambazo niligusia mpaka na kifungu sasa nataka niende katika mswada huu. Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba Mwanasheria Mkuu yeye ndiye mshauri mkuu wa serikali yetu na tunaposema kwamba mshauri mkuu wa serikali yetu ndiye mshauri mkuu kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, hii nafasi Mhe. Spika, sio nafasi ndogo hii ni nafasi kubwa sana, kwa sababu mikataba yote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakayosainiwa ikiwa ya ndani au ya nje basi Mwanasheria Mkuu ana dhima kubwa sana, tukipata mikataba mibovu basi itakuwa Mwanasheria Mkuu hakuisaidia serikali, tukipata mikataba iliyo bora basi Mwanasheria Mkuu atakuwa ameweza kutusaidia sana kwa serikali.

Sasa Mhe. Spika, kitu ninachoataka kukizungumza kwamba hivi sasa tumekuwa kila taasisi inakuwa ina wanasheria wake na wanakuwa na mamlaka yao ya kuweza kuamua vile ambavyo wanahisi wao. Mhe. Spika, tumeshuhudia kuna baadhi ya mikataba inafungwa ndani ya mawizara yetu lakini mikataba ile baadae inakuja kuitia hasara serikali. sasa hii inaonesha kwamba mikataba ile ilipokuwa inafungwa tunakuwa hatukuwa na umakini wa kutosha, lakini kwa kuwa sasa hivi tunaunda hii sheria na tayari kuna vifungu ambavyo tumeshampa Mwanasheria Mkuu kuweza kusimamia shughuli zote za serikali na vile vile kuweza kuwaongoza na kuwaelekeza kwamba sasa hivi Wanasheria wote hawatakuwa na mamlaka ya kuweza kufanya kazi yakufunga mikataba bila ya kupata ushauri na idhini ya Mwanasheria Mkuu.

Hii Mhe. Spika, ndio katika ile kutekeleza *Vision 2020* pamoja na MKUZA, sheria hii ndio inakuja kusimamia zaidi katika kutekeleza ule MKUZA. Kwa sababu tukiwa na mikataba mizuri Mhe. Spika, *automatic* fedha za umma zitatumika vizuri, mikataba itatumika vizuri kwa hivyo hakuna fedha zitakazoweza kupotea ovyo.

Lakini vile vile hata katika suala la miradi yetu wakati mwengine tunakuwa na miradi yetu inakufa njiani, inaharibika njiani, hii inatokana kwa sababu gani, kutokana na kutokuwa makini katika ile mikataba. Kwa hivyo, Mwanasheria Mkuu kwa kweli sasa hivi atakuwa na kazi kubwa lakini vile vile nawaomba na taasisi nyengine za serikali hasa kwenye mashirika wampe mashirikiano Mwanasheria Mkuu, kwa sababu kama tunavyojua wanao wanasheria wao sasa kwa kuwa walikuwa wako huru katika kufanya mambo yao lakini sasa hivi kutakuwa na *controller* ambaye anaweza kuyadhibiti tena isije ikaaza kuwa nongwa, kwamba oo sisi tunasema hivi yeye anasema hivi.

Kwa kuwa tunapitisha sheria Mhe. Spika, kama tunavyosema siku zote kwamba tunaomba hii sheria tutayoipitisha basi iweze kutekelezwa na isimamiwe ipasavyo. Hatutegemei kuanzia sasa hivi baada ya Mhe. Rais kutia saini sheria hii kwamba tayari kutakuwa na mambo ya kiajabu ajabu ambayo yataweza kutokezea katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka Mwanasheria Mkuu anapokuja kutoa ufafanuzi anisaidie jambo moja, kwa kuwa sisi ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa katiba tumeipa mamlaka ya kuridhia mikataba ya kimataifa na kama tunavyofahamu kwamba mikataba ya kimataifa ikishasaini Tanzania ina maana *automatic* na Zanzibar tayari tumeshakubali masharti yale.

Sijui hivi sasa utaratibu uko vipi, kama ile mikataba ya kimataifa inaporidhiwa sijui kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar inashirikishwa kikamilifu katika maandalizi ya kuangalia mikataba ile na baadae hatima yake kuridhia ambapo ikiridhia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar tunakuwa tumesharidhia. Je, utaratibu huo ulikuwa unafanywa? Kama ulikuwa haufanywi tunaweza tukatengeneza vipi sheria ili sasa hivi mikataba yote ya kimataifa tangu kuanza *process* za kuanza kufuatilia na kuangalia yale masharti Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu kuipa mamlaka ya kuweza wao kushiriki kikamilifu na kuweza kuridhai kwanza kabla ya kuipa mamlaka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia mikataba hii.

Mhe. Spika, kwa sababu katika mambo ya kuridhia mikatata hii kuna mambao mengine yanakwenda na mila, silka na utamaduni wa nchi husika. Kama tunavyofahamu tamaduni zetu zinatofautiana baina eneo moja na eneo jengine. Sasa tusije tukaridhia mikataba halafu baadae kuna sheria zinazotaka kutekelezwa tukajaanza kumbana Mwanasheria Mkuu. Sasa hapa nilikuwa nataka kidogo aje anisaidie vipi ushiriki wa Zanzibar katika kuandaa mpaka kuweza kuridhia mikataba ya kimataifa.

Kwa sababu Mhe. Spika, tunajua tuna Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo ina idara inaratibu shughuli za Muungano. Mtume Muhammad (SAW) du!

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe endelea tumepata taarifa kwamba kumekuwa na hitilafu kidogo lakini bado tuko salama kwa hivyo endelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nimekubali kuendelea lakini natoa ushauri hii nje ya mswada. Mhe. Spika, leo nilikuwa katika ofisi yetu ya utumishi kwa kina Biubwa kule unajua shughuli gani tunazokwenda kuzifanya, Mheshimiwa taa zilidata tulitoka mbio mlango mmoja tukanyang'anyiana watu wawili. Sasa inaonesha ndani ya Baraza letu kuna *shock* na leo taa ndio imepasuka hapo kwa bahati nzuri haikuja kuanguka huko kwako. Sasa nilikuwa naomba ofisi yako Mhe. Spika, iwasiliane na wenzetu wa Shirika la Umeme kuja kuangalia kuna

hitilafu gani, kwa sababu milango yetu ya kutokea sijui iko mingapi, sasa hilo kidogo Mhe. Spika, naomba tulichukue.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulizungumza kwa kuwa tunaanzisha sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu sasa kuna mambo hivi sasa yanafanyika Mhe. Spika, nitaomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu atusaidie sana. Wakati mengine ukiacha haya masuala ya wizara moja kwa moja, lakini tuna Halmashauri na tuna Mabaraza ya Miji kule kuna wanasheria, wakati mwengine Mhe. Spika, kuna *notice* zinatolewa, kwa sababu mimi kamati yangu inasimamia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo Serikali za Mitaa ziko chini ya usimamizi wa kamati yangu…

Mhe. Spika: Nimepewa taarifa na mafundi wetu kwamba hitilafu hii ya umeme inaonekana ni kubwa na hapa na pale taa zimekuwa zinaleta hitilafu na hatujui kitakachoendelea. Kwa sababu ya dharura hiyo naona niahirishe kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 08/04/2013 saa tatu za asubuhi.

(Saa 12:26 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 08/04/2013
Saa 3:00 asubuhi)